

KUONEA HAYA



Asante, Ndugu Neville. Ubarikiwe!

Habari za asubuhi, marafiki. Ni vyema kuwapo hapa asubuhi hii. Nami nafikiri nilifanya ninii... Mimi ni mvamizi wa muda wa Ndugu Neville. Akiketi huko nyuma na ninii lake, akilitayarisha somo lake; nami nikaingia, alianza kulifunga somo lake, na kusema, “Vema...”

² Inanikumbusha juu ya miaka kadhaa iliyopita. Kulikuwako na ndugu mmoja mweusi hapa, anayeitwa Ndugu Smith, na Dada Cross. Walikuwa ni marafiki wangu wazuri sana. Na wakati ningeingia jengoni usiku, jamaa huyo mzee alikuwa... Alikuwa na masharubu meupe. Sijui kama yeyote wenu anamkumbuka, ama la. Naye angekuwa jukwaani, mwajua. Na wote wangekuwa wakiimba, “Ni Njia Kuu ya Kwenda Mbinguni.” Basi Ndugu Smith, anaketi tu namna *hii*, unajua. Nami ningeingia kwa mlango wa nyuma.

³ Kulikuwa na msichana mdogo, kwa namna fulani mweusi sana, alikuwa ana tabia ya kukaa pembeni. Angeanza kupiga makofi, akisema, “Mwinueni,” wimbo huo, unajua. Wanaweka sauti yao wenyewe ndani yake, mwajua. Halafu huko kwenye kona ya pili, kutakuwako na mtu mwingine, anasema, tuimbe tena, “Mwinueni.” Vema, huo ndio wangeuimba wakati nikiingia mlango. Ninalipenda sana kundi hilo la watu.

⁴ Na kwa hiyo mzee Ndugu Smith angeketi kule nyuma, kidogo, unajua, naye alikuwa kwa namna fulani mtu mnyamavu. Angesema, “Karibu, mzee, pumzisha kofia yako.” Sio “jipumzishe”; “pumzisha kofia yako,” unaona. “Karibu, mzee, pumzisha kofia yako.” Angesimama pale, na, ningeweza kujua jinsi alivyoanza, nilikuwa nimepatikana, unaona.

⁵ Angesema, “Vema,” anasema, “watoto, mnajua,” akasema, “Ni—nilikuwa tu nimeketi hapa nikishangaa, ‘Bwana, utanipa nini la kusema?’” Kasema, “Yeye—Yeye—Yeye akaendelea kukitikisa kichwa Chake, kunitikisia kichwa Chake. ‘Sitakupa chochote cha kusema.’” Kasema, alisema, “Nimemwona Mzee Branham akiingia kule nyuma, nami nikasema, sasa, ‘Bwana, ndio tu ninaanza kukumbuka...’” Vema, papo hapo nilikuwa nimepatikana!

⁶ Ndugu George Wright, u hali gani, ndugu? [Ndugu Wright anasema, “Loo, niko vizuri. Hakika.”—Mh.] Ubarikiwe, Ndugu Wright! Hakika. [“Ndugu Elijah yuko kule nyuma.”] Loo, hiyo ni kweli? Ndugu Elij’ Perry, alisema, yupo hapa nyuma. Uko wapi, Ndugu Elij’? Sijamwona kwa ninii mrefu... Vema, jamani, saa! Sasa inatupasa kufanya mkutano kwelikweli hapa! Elij’ Perry, George Wright, na baadhi ya hao watu wa zamani waliokuwa

hapa wakati karibu ilikubidi kushikilia vilango mahali pake, kwa mikono yetu, upepo ukivuma. Nafurahi kukuona! Mama, Dada Wright yuko pamoja nawe? Dada Wright yuko humu? Yuko huko nyuma, pia. Naam, bwana. Vema, ni vema jinsi gani! Dada Perry, ninawaona wote sasa. Vema, kweli hilo ni jambo zuri. Ni vema kuwa humu. Ni vema kuketi sehemu hizi. Ni vema kuwa pamoja.

⁷ Nilikuwa nimepanga, kwa bidii sana, kurudi; mzungu moyoni mwangu. Ndiyo kwanza nirudi kutoka Afrika, kama mjuavyo nyote. Na nilipofika kule, nilikuwa na visa yenye masharti, nao wasingeniruhusu, wasingeniruhusu kuhubiri kwa sababu inawakusanya watu wengi kupita kiasi. Wanatarajia maasi kule wakati wowote, na—nao—wasingeniruhusu kuhubiri kwa sababu ya huko kukusanyika watu wengi kupita kiasi. Njia pekee ningaliweza, ingekuwa ni kupata shirika fulani ambalo limewakilishwa na serikali, katika serikali, linialike huko, basi hilo mara moja lingeliifanya serikali kutuma wanamgambo kwa ajili ya ulinzi. Mnaona, wao wananinii tu. . . Kutakuwako tu na maasi, na ni hayo tu katika hilo. Yako karibu sana, unaona. Huyu mtu wa serikali alisema, “Mara ya mwisho alipokuwa hapa, aliwakusanya karibu watu nusu milioni.” Kisha akasema, “Basi, unaona, hicho kingekuwa ndicho kitu hasa ambacho ukomunisti unatafuta, kwa ajili ya maasi.” Kwa hiyo, nisingeweza kuhubiri.

⁸ Hao watu wakisimama huko, wakipunga mikono yao, na kupaza sauti, “Mkumbuke mama yangu! Kumbuka, ndugu yangu alikufa! Nanii wangu. . .” Huko, na nyuma ya kizuizi, mwajua, vizuizi vya waya, na lilikufanya tu ujisikie vibaya sana. Basi nikarudi nyumbani.

⁹ Ndipo nikawaza, “Vema. . .” Mwanangu, Joseph, ambaye yuko huko nyuma, alikuwa amelegea kidogo katika masomo yake. Naye alikuwa. . . Kweli alifaulu, lakini ilimbidi kurudia; hakuwa akisoma vizuri vya kutosha. Kwa hiyo nikawazia, “Vema, itatubidi kukaa nyumbani kwa muda kidogo.” Kisha nikasema, “Kama tukikaa nyumbani, itavuruga likizo ya watoto.” Kwa hiyo tukaiahirisha tu, na kumpeleka mahali pengine Agosti, na kuacha. . . ndipo tukaja hapa kwa majuma kadhaa, majuma matatu.

¹⁰ Nikasema, “Ninaamini, wakati tukiwa tumerudi huko, nitachukua tu na kufanya mkutano. Tutapata lile jumba la mikutano la shule hapa juu, na—nasi tutafanya mkutano kutoka tarehe ishirini na nane mpaka tarehe moja, mkutano kwenye ukumbi wa shule. Nilitaka kuhubiri juu ya somo la kumwagwa kwa vile Vitasa saba vya mwisho.” Na kwa hiyo tukapiga simu mapema, nasi tukapata kuvunjika moyo kidogo. Hawataturuhusu kuchukua shule hizi tena, watu wengi sana kupita kiasi wanasongamana mle. Hatuwezi kuufanya popote. Na kwa hiyo basi nikaamua, wakati nilipokuwa nimerudi hapa basi, badala ya. . .

¹¹ Hatuwezi kuwaweka watu wote, kama tungetanga... Haujatangazwa kamwe, sasa. Kwa hiyo kama tukiwaweka watu wote, tukijaribu kuwaweka kwenye maskani hapa, tusingeweza kuwaweka. Mnaona, ni ninii tu... siku tano hapa zingekuwa ni jambo baya sana.

¹² Kwa hiyo, nikiwa nimeketi pale ndani nikizungumza na Ndugu Neville na Ndugu Wood, na hao wengine, tumeamua kufanya jambo hili. Kama hatuwezi, badala, hilo lingetufanya tuwe na ibada tano; hiyo ingekuwa ni tarehe ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini, thelathini na moja, na tarehe moja. Vema, ninaona kama tukiifanya, kuanzia Jumapili ijayo, tunaweza kufanya ibada mbili, Jumapili asubuhi na Jumapili usiku, hiyo ni tarehe kumi na nane. Halafu basi kwenye ninii—kwenye tarehe ishirini na tano, tuwe na Jumapili asubuhi na Jumapili usiku. Hizo ni ibada nne. Halafu kwenye tarehe moja Agosti, tuwe na Jumapili asubuhi na Jumapili usiku. Hilo lingetupa ibada sita, ndipo haitasababisha msongamano mkubwa kuwaingiza watu ndani. Basi ninawazia hilo.

¹³ Hivi hamwoni hiyo ingekuwa ni bora zaidi kuliko kumfanya kila mtu kusongamana na kubanana, na kila kitu? Halafu hilo tu kwa ibada hizo mbili, tunaweza kuvumilia hilo, lakini kila mtu kwa namna fulani ashirikiane. Muda wa siku tano usiku, mfululizo, ingelifanya kuwa gumu.

¹⁴ Nami nataka kukutana na wadhamini na wazee hapa, wakati nikiwa hapa.

¹⁵ Hili linatukia kila mahali. Tunaishi katika siku hizi za mwisho, ambapo Injili haina ma—mamlaka kama inavyopaswa kuwa nayo. Haina haki inavyopaswa kuwa nazo. Yote imeshikamanishwa katika siasa na kadhalika, na kama tu muungano. Na huo ndio inaoelekea hatimaye kufikia, kwa maana ile alama ya mnyama haina budi kuja kwa muungano, tunajua. Kwa hiyo sisi—sisi... Maana, ni kususiwa, “hakuna mtu anayeweza kununua wala kuuza, isipokuwa yule aliye na alama ya mnyama.”

¹⁶ Na sasa ninataka kujua, kupitia kwa wazee. Ninajisikia kuongozwa. Sijapata kuwa na njaa kama hiyo moyoni mwangu kwa ajili ya Mungu, maishani mwangu mwote, kuliko niliyo nayo sasa, unaona. Kwa kuwa... Na mimi—mimi nataka kupata hema langu mwenyewe na vitu vya—vyangu, kama vile Mungu alivyonipa ono, nami ninaamini wakati umewadia sasa. Na ninataka kuona wakati nikiwa hapa, ni kwa nini hatuwezi kupata hema hilo.

¹⁷ Na—na halafu wakati tunapoondoka, kama vile kuja hapa Jeffersonville, badala ya kuwa tu na siku moja ama mbili, ama siku tatu ama nne, tunaweza kutoka hapa nje na kupiga hema hili, na kuwa na majuma mawili ama matatu, mnaona, na kamwe hakuna mtu anayeweza kusema lolote juu yake. Tunaweza

ama kuchukua uwanja wa mpira, au, kama hawataturuhusu kuuchukua huo, yupo mkulima hapa kijijini atakayeturuhusu tutumie shamba moja. Tatalikodisha shamba hilo na—na kupiga hema. Jambo pekee litakalotulazimu kufanya kule, lingekuwa ni kujenga majengo yetu—yetu ya nje, na kadhalika, na kwa manufaa yetu. Na hilo lingeweza kufanywa kwa urahisi. Ndipo tutaanza kufanya ibada zetu jinsi hiyo kwa kuwa hiyo ni kulingana na ono kutoka kwa Bwana, na inapaswa kufanywa hivyo.

¹⁸ Na wakati nikiingia, jana, na kukuta, wajua, *hili, lile*. Nami nilikuwa nikipanda barabarani, na rafiki yangu msiri akienda pale, kasema, “Halo, Billy.” Nikamwangalia, na nywele nyeupe kama theluji, tumbo kubwa *hivyo*. Na mvulana huyo ni wa rika langu. Tulicheza pamoja, mtu kijana mwenye sura nzuri, nilipokuwa mtoto. Kwa namna fulani ilinifanya kujisikia asiye wa kawaida.

Mwanangu mdogo, Joseph, alisema, “Mbona una huzuni, Baba?”

¹⁹ “Loo,” nikasema, “siwezi kulielezea kwako, Joseph. Unaona, siwezi, siwezi kukwambia.”

²⁰ Ndipo nikamwangalia Elij’ Perry ameketi kule nyuma, na Bibi Perry; inaonekana kama jana walikuwa ni mume na mke wadogo wenye nywele nyeusi kule walikokuwa, wakiishi jirani yangu, wakati tulipokuwa na ule mtumbwi wa kale, Wahoo, na huko chini mtoni na kuvua samaki usiku. Nawaona wote wawili wana mvi, unajua, inanena jambo moja, ni mvumo mdogo unaosema, “Huna wakati mwingi zaidi.” Unaona?

²¹ Kwa hiyo, ninataka kila siku ya maisha yangu ihesabiwe Kwake. Ule uliosalia kwangu, ule wakati nilio nao, ninataka kuutumia mahali fulani nikifanya jambo fulani, kama si zaidi ya kusimama pembeni mwa mtaa fulani, nikishuhudia kwa ajili ya utukufu na heshima ya Mungu. Na mimi—mimi nipo hapa kwa kusudi hilo.

²² Na nina mahali pa siri hapa juu kwenye Kinu cha Green, Indiana. Sio jiji, sasa, ni—ni nyika. Na watu wengine wanapamiliki, na hata hawatakuruhusu upakanyange mguu mmoja. Bali nina pango pale ambamo asingeweza kunipata nikiisha kuingia ndani yake. Mimi huingia usiku, na kamwe hatajua wakati nikiingia au kutoka. Wala hajui mahali pango hilo lilipo, wala asingelipata haidhuru lilikuwa wapi. Nami ninataka kwenda kule na kusema na Bwana, kidogo, ninajisikia ya kwamba hilo linahitajika.

²³ Mke wangu, anataka kuja, anataka kurudi na kutembelea huku, na Rebekah na Sara, na wao wengine, pamoja na marafiki zao. Nasi tumerudi hapa sasa kwa majuma matatu yajayo, na kama Bwana akipenda.

²⁴ Nami nafikiri, badala ya kujaribu kuwasongamanisha watu pamoja, kwa ajili ya hiyo mikutano hapa maskanini . . . Hakika, hii ni yetu, ni ya Bwana, alitupa sisi. Nayo imeyoyozwa. Ningependa kufanya ibada ya Jumapili asubuhi, ibada ya Jumapili usiku. Hiyo ingewawezesha watu warudi makwao, kisha wangojee mpaka juma lijalo.

²⁵ Sidhani ningeweza kuchukua na—na kushughulikia vizuri kule kumwagwa kwa vile Vitasa vya mwisho, maana hivyo, hivyo ni Ujumbe mkubwa mno humo ndani. Lakini ningeweza kuwaombea wagonjwa, na kufanya mambo ambayo . . . nina Jumbe, pia, kama Bwana atakavyonipa, kwa ajili ya kanisa. Kote katika juma hili, nitaingia hapa nje nyikani mahali fulani na kusoma, nirudi Jumapili asubuhi, nifanye ibada ya Jumapili asubuhi namna hii, na ibada ya Jumapili usiku. Maskini mchungaji wetu mwenye rehema sana, Ndugu Neville, nilimuuliza kama hiyo ingemridhisha. Hilo ni kumnyang'anya ibada zake zote, bali alikuwa na furaha zaidi kuziachilia kwa—kwa hizo. Ninaninii tu . . .

²⁶ Ndugu Capps, yeye, nadhani, ana homa ya kutangatanga, pia, na ninaona ameondoka, na—na Ndugu Humes. Naye Bwana alikuwa na Ndugu Mann hapa kuchukua moja kwa moja, pia mahali hapo. Mwajua, si ni ajabu jinsi Bwana atakavyofanya mambo? Daima Yeye ana kila kitu kwa wakati unaofaa kabisa. Nilikuja huku nikamsikia mtu fulani akihubiri. Nikasema, “Hiyo haininii . . . Ninaamini . . .”

²⁷ Ndugu Capps, alikuja Tucson, nami nafikiri lilimduwaza upesi sana, ilikuwa ni kama digrii mia moja na kumi. Hakupenda jambo hilo, kwa hiyo huyoo akaondoka zake, yeye na Ndugu Humes, nao wakaenda hadi Phoenix. Bila shaka, ni digrii mia moja na kumi na tano hadi kumi na sita, kumi na nane kule juu. Hiyo ilikuwa ingali ni mbaya zaidi, kwa hiyo nafikiri aliondoka akaenda Texas baadaye; yeye, akijaribu kupata mahali.

²⁸ Lakini hutaki Arizona yoyote wakati huu wa mwaka, nakwambia. Ilikuwa ni mia moja na arobaini, hivi majuzi, Ijumaa iliyopita, digrii mia moja na arobaini, huko Parker. Na hapo ndipo Ndugu Craig, kutoka hapa kanisani, anapoishi. Nawe unaweza kulivunja yai, nalo litaiva kabla halijagusa chini. [Ndugu Branham anacheke—Mh.] Mtu, unatema mate na—na unyevu umekwisha, inaninii tu . . . Hakuna unyevu wala chochote kile, kwa kweli ni jiko la kuokea wakati huu wa mwaka. Lakini kutoka kwenye kama Novemba, Desemba na Januari, kuzuri sana. Lakini inapofikia karibu na Marchi na Aprili, ni heri uondoke kama hutaki kukosa hewa.

²⁹ Na kwa hiyo ilitokea kwamba Ndugu Capps na hao wengine walikuja tu kwenye wakati huo, ambalo nafikiri liliwafukuza. Kwa hiyo pengine Bwana alifanya hivyo kwa kusudi fulani.

Ninaamini jambo hili, ya kwamba Mungu huamuru hatua za wenye haki. Wakati mwingine huonekana ni jambo gumu.

³⁰ Kama vile hivi majuzi kwenye safari hii ya Afrika, nilikuwa na hakika kabisa ya kwamba nilikuwa nikienda katika mapenzi ya Mungu. Kwa sababu, mwaka mmoja uliopita, nilikuwa huko chini Kusini, nikiendesha mfululizo wa mikutano, na, wao—wao, nilidhani . . .

³¹ Nikitoka kwenye shirika hilo, walisema, “Unaweza kuja, kupitia kwa Wafanya Biashara Wakristo, bali sisi hatutakuwa na uhusiano wowote nalo.”

³² Vema, sitaki kuwaingiza watu hao moja kwa moja ndani ya jambo hilo, mwajua, kuleta ugomvi. Ni—ninataka kuwafanya wajisikie vizuri wao kwa wao. Kwa hiyo nilisema tu, “Vema . . .” Nikawaandikia barua, nikasema, “Kumbukeni, nimejaribu kuingia Afrika kwa miaka mingi, tena, nikijisikia ya kwamba huduma yangu haijaisha Afrika. Sina . . .”

³³ Kwa nini inibidi kwenda Afrika, wakati nikiwa na miji mia sita, mia saba papa hapa Marekani, inaniita, mnaona, mumu humu tu, bila ya kuacha Canada, Meksiko, ama moja ya mahali popote pale? Kwa nini niwe na shauku ya kwenda kule? Lakini ni kitu fulani moyoni mwangu, kinachonivuta niende Afrika. Kule, watu hao, kuna—kuna jambo fulani kuwahusu, ambacho nakipenda, nami ninataka kwenda kwa ajili ya watu weusi peke yao. Na kuna jambo fulani katika wengi wao, hao viongozi, hawajisikii kwamba ninapaswa kufanya hivyo. Na—nataka kwenda kwa rafiki zangu weusi. Huko ndiko Bwana alikoniitia. Na sasa wao ni wahitaji. Wengi wa watu hao, hao wazungu, wanaweza kuwa na madaktari na kila kitu. Lakini hao wenyeji maskini wanaishi kule, na wameoza nusu. Mimi—mimi—mimi najisikia hao ndio wanaonekana kana kwamba wangeupokea. Hao ndio. Kuna kitu fulani kuhusu jambo hilo.

³⁴ Unapofikia mahali, wewe ni mwereru sana hata unajua kila kitu, basi Mungu hawezi kufanya lolote nawe. Lakini ukifikia mahali ambapo uko tayari kusikiliza na kujifunza, basi—basi ni wakati wa Mungu, anaweza kuingia na kuzungumza na wewe.

³⁵ Na kwa hiyo niliwaandikia barua, na kuwaambia. Nami nikasema, “Kumbukeni, kwenye ile Siku ya Hukumu, acheni hiyo mikono iliyokonda sana itokeze kwenye ule moshi, ikawahukumu! Damu yao na iwe juu yenu, sio juu yangu, maana nimejaribu kwa karibu miaka kumi kurudi.”

³⁶ Ndipo wakati nilipoituma barua hiyo, nikarudi, Kitu fulani kiliniambia, “Kamwone Sidney Jackson, fanya safari ya kuwinda.” Na, wakati uo huo, Bwana akasema na Sidney Jackson, akasema, “Simba mwenye manyoya ya manjano, Ndugu Branham kufanya kambi; Durban, mkutano mkubwa.”

³⁷ Vema, alikuwa hapa, naye akasema nanyi hapa. Jambo lingine, tulibatiza . . . Alikuwa akipinga kwa dhati ubatizo huu

katika Jina la Yesu Kristo. Na mke wake alikuwa mbaya kuliko yeye alivyokuwa, yeye angeondoka tu. Ungeweza... Ninawaambia, sijapata kuona watu wenye bidii zaidi. Wana kama wahudumu mia moja na hamsini kule, waliobatizwa katika Jina la Yesu Kristo, nao wanaiwasha tu moto nchi hiyo. Ujumbe huu unaenea upesi sana Afrika, kila mahali, marubani na watu mashuhuri wanakuja, wakibatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

³⁸ Na kwa hiyo mimi, wakati nilipoanza kwenda kule, ninawaambia, kamwe sijapata kuwa na shida nyingi jinsi hiyo maishani mwangu mwote, ya kujaribu kuingia kule. Halafu basi dakika ya mwisho kabisa, dakika ya mwisho kabisa ya kwenda, visa yangu ikaandikwa hivi, “Hawezi kuhusika kwenye ibada ya aina yoyote ya kidini; anaweza kuja tu kuwinda.” Vema, basi, ilikuwa mbaya kweli.

³⁹ Lakini nikasema, “Sijali yale ibilisi afanyayo, si—siwezi... Siwezi kutetea yale Ndugu Jackson alisema kuhusu simba mwenye manyoya ya manjano, na *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Si—siwezi kulitetea. Lakini ninajua Mungu aliniambia ni-‘mwone Sidney Jackson, na mwende mkawinde.’” Ndipo nikasema, “Ninaenda.” Na wakati mwingine... Basi nilikuwa na moja ya safari nzuri mno.

⁴⁰ Niligundua shida ilikuwa ni nini. Sasa nafikiri, kama Oktoba, Bwana akipenda, ninaweza kurudi na kufanya mkutano na kila kitu, ushirikiano mkamilifu, kila kitu kingine, mnaona, huko Afrika sasa. Nililiingilia kindani na nikaona ilikuwa ni wapi, kile kilichoisababisha. Hapa juu, akiandika, huyu ana *hili* la kusema, na kitu fulani kina jambo la kusema, na *huyu* pale. Jambo zuri sana la kufanya, ni uende ukatafute kujua, wewe mwenyewe. Nami ninajua mahali shida ilipokuwa, na sababu yake ilikuwa ni nini; ilikuwa ni kwa sababu ya kukusanyika kwa watu wengi sana pamoja, serikali isingeniruhusu niifanye.

⁴¹ Sasa kama Wafanya Biashara Wakristo ama shirika lolote, ndilo litakalotuingiza, basi serikali mara moja... kwa sababu shirika hilo limewakilishwa kwa serikali, serikali itatuma wanamgambo walenzi. Kama kungekuwako na watu ishirini na watano kutoka kwenye dhehebu moja, ishirini na watano kutoka kwa lingine, wangali hawatapokea hilo. Haina budi kuwa ni ki—kiongozi wa shirika hili. Nalo shirika la Wafanya Biashara Wakristo si la kidhehebu na linawakilisha makanisa yote. Daktari Simon, kiongozi wao huko, mtu mzuri sana, niliweza kukutana naye na kuzungumza naye. Nao wanaichukua mikutano hiyo, na makanisa yote mengine yanakusanyika pamoja. Mnaona? Nami ninaamini tutakuwa na mmoja wa mikutano mikubwa mno ambayo imewahi kufanyika Afrika.

⁴² Lakini wazo langu lilikuwa ni hili, wakati unapojua ya kwamba u—unajaribu kufanya jambo lililo sahihi, jambo la

kwanza ni, kama ukijisikia kuongozwa kufanya jambo lolote, basi lihakikishe na Neno na uone kama ni sawa na Neno, na halafu usiache chochote kikuzuie. Sijali ni magurudumu mangapi ibilisi anayatupa njiani, yaruke tu moja kwa moja.

⁴³ Nilimwambia mke wangu na nikamwambia Ndugu Wood, nilipofika hapa, na baadhi ya marafiki niliokutana nao jana: Nimekuwa na karibu miaka mitano hapa ambapo karibu sikujua la kufanya. Imekuwa ni wa—wasiwasi... Mnaona, uamsho wenyewe, miongoni mwa makanisa, ulikuwa umekufa. Kila mtu anajua jambo hilo. Unalihisi humu maskanini. Unalihisi kila mahali. Kuna mshindo mzito mno, wa mauti. Kuna kasoro fulani tu. Ni kwa sababu ile hamu ya uamsho imewaacha watu. Ukiingia makanisani, utawaona wameketi pale. Naye mchungaji anatutusa-tutusa apate ujumbe ama chochote kile. Na muda si muda wajua, anaukatiza kwa ajili ya namna fulani ya karamu wanayotaka kufanya, ama chochote kile. Inaonekana ni mshindo mzito sana uliokufa kila mahali.

⁴⁴ Billy Graham analiona; Oral Roberts. Bw. Allen alikuwa na matatizo fulani, kama mjuavyo. Oral Roberts ana majengo ya dola milioni hamsini, na kadhalika, mle ndani. Ana shule. Na, vema, hakuna mtu aliye hudumani sasa.

⁴⁵ Niliondoka hapa, kwa ono, kwenda huko Tucson, kuona yale Bwana aliyotaka nifanye. Huko alikutana na mimi kule, kama vile alivyowaambia hapa kuwa angefanya, na umbo la Malaika saba, kisha kasema nirudi huku na ile Mihuri Saba itafunguliwa. Hilo hasa ndilo lililotukia.

⁴⁶ Akasema, siku moja tukiwa na Ndugu Wood wakati alipokuja huku nje, tulienda mahali pale pale, ndipo nikatupa jiwe juu, likarudi chini, Yeye akasema, “Katika siku moja mchana na usiku, mtaninii...” Baadhi, ninasahau maneno yenyewe hasa yalikuwa ni maneno gani. “Utauona utukufu wa Mungu.”

⁴⁷ Na kesho yake, upepo wa kisulisuli ulishuka chini kutoka angani, nasi tunajua hadithi ya yale yaliyotukia. Wakati ulipopaa juu, wao waliuliza ilikuwa ni kitu gani. Nikasema, “Ilinena maneno matatu, katika milipuko mitatu mikubwa.” Hao watu walisikia tu hiyo milipuko. Mimi nilifahamu yale iliyosema. Nayo ilisema, “Hukumu inaipiga Pwani ya Magharibi!” Siku mbili baada ya hapo, Alaska nusura izame. Yamekuwa yakinguruma kila mahali, matetemeko ya nchi, kila kitu. Hebu yaangalie tu, kila siku, matetemeko ya nchi yakitikisa kila mahali.

⁴⁸ Mkutano wangu wa mwisho, mkutano wa mwisho niliokuwa nao, huu utakuwa ndio Ujumbe wangu wa kwanza, hasa, kuhubiri tangu wakati huo. Nilikuwa nikihubiri huko Los Angeles, kwenye Ukumbi wa Biltmore, nami nilikuwa nikizungumza juu ya mwanamume kujichagulia mke. Labda

mlipata kanda yake. “Inaninii,” nilisema, “Inaonyesha tabia na malengo yake.” Kwamba, mtu anapomchukua mwanamke, anapomchukua msichana mdogo, na ili awe mke wake; akimchukua, unajua, msichana wa kisasa ambaye ni Riketa wa kupendwa na wengi, i—inaonyesha tu kile alicheo... Kama akimwoa mshindi wa shindano la urembo ama malkia wa kuvutia kimapenzi, yeyote yule, inaonyesha ninii yake, kile hasa kilicho ndani ya mtu huyo. Lakini Mkristo, yeye huangalia tabia katika mwanamke, kwa sababu yeye anapanga makao ya usoni pamoja na mwanamke huyo. Anapanga, anampata mtunza nyumba. Nami nikasema, “Basi, Kristo, kulingana na Neno Lake hapa, anatwambia jinsi Makao yetu ya usoni yatakavyokuwa. Yeye atachagua mke wa aina gani basi, kahaba wa kimadhehebu? Hasha! Atachagua mwanamke aliye na sifa za Neno Lake, na huyo atakuwa ndiye Bibi-arusi.”

⁴⁹ Na wakati tukiwa mle ndani, Kitu fulani kilinigusa, nami sikujitambua kwa karibu dakika thelathini. Kulikuwa na unabii uliotolewa. Jambo la kwanza ninalokumbuka, Ndugu Mosley na Billy, nilikuwa huko nje mtaani, nikitembea. Ndipo huo ukasema, “Ewe Kapernaumu, ambaye unajiita kwa jina la Malaika,” hilo ni Los Angeles, jiji la malaika, unaona, malaika, “ambaye umeinuliwa hata mbinguni, utashushwa chini hadi kuzimu. Kwa maana, kama hizo kazi kuu zingalifanywa Sodoma, ambazo zimefanywa kwako, ungalikuwa umesimama hata siku hii.” Na hayo yote yalikuwa bila fahamu kwangu, mimi. Unaona?

⁵⁰ Na jinsi ambavyo ndiyo kwanza nimalizie kuwasihi, Kristo, nikimwinua Yeye na kuliambia kanisa. Nikasema, “Enyi wanawake, haidhuru ninajaribu jinsi gani kuwajia, ama kuhubiri dhidi ya mambo haya; nanyi wanaume, enyi wahubiri; mlichunguza wakati wote, mnalifanya vivyo hivyo. Mnalipuuza kana kwamba Neno la Mungu halikuwa kitu.”

⁵¹ Basi wakati nilipolielewa jambo hilo, nilienda, nikasema, “Kuna Andiko juu ya jambo hilo mahali fulani.” Basi nikaenda na kuona ilikuwa ni Yesu, akiukemea Kapernaumu karibu na pwani ya bahari. Usiku huo niliyaangalia Maandiko. Nikaja nyumbani, nikachukua kitabu cha historia; na Sodoma na Gomora wakati mmoja ulikuwa ni mji u—ulioostawi, makao makuu ya Mataifa ya ulimwengu. Nanyi mwajua, jiji hilo, kwa tetemeko la nchi, ulizama katika Bahari ya Chumvi. Na Yesu alisimama, na kusema, “Kapernaumu, kama Sodoma ungalifanyiwa kazi ulizofanyiwa wewe, ungalikuwa umesimama hata sasa. Lakini sasa huna budi kushushwa hata kuzimu!” Na yapata miaka mia mbili ama mia tatu baada ya unabii Wake, huku miji hiyo yote ya pwani, kila mmoja ukiwa ungali unasimama ila Kapernaumu, nao uko chini ya bahari. Tetemeko la nchi liliuzamisha chini ya bahari.

⁵² Na kisha kutabiri, “Los Angeles itakuwa chini ya bahari.” Ndipo nikaja nyumbani, na nikaenda Afrika. Na wakati nilipokuwa Afrika, walikuwa na tetemeko la nchi. Nao wanasayansi... Mliona jambo hilo, ilitangazwa, kwamba baadhi ya majumba makubwa, mazuri yalididimia ndani, huko Los Angeles, na moteli moja, na kadhalika. Na sasa kuna ninii...

⁵³ Tangu tetemeko hilo la nchi, kuna mwatuko wa inchi mbili ama tatu ulioingia ardhini, ukianzia huko Alaska, unazunguka kupitia kwenye visiwa vya Aleutian, unatokea yapata maili mia moja na hamsini ama mia mbili baharini, unarudi San Diego; unaimeza California, ama Los Angeles, kisha unatokea tena chini tu ya sehemu ya kaskazini mwa California pale, mahali padogo panapoitwa San Jose, kule chini tu.

⁵⁴ Naye mwanasayansi huyu alikuwa akizungumza, akiwa kwenye mahojiano. Tulikuwa tukiangalia kwenye televisheni. Ndipo akasema, “Chini ya huo ni lava tupu inayotibuka.” Ndipo akasema hivi, akasema, “Kipande hicho kikubwa kitaachilia,” kisha kasema, “na kitaachilia.” Na haya maho-...

⁵⁵ Mtu huyo, mwanasayansi akimhoji mwanasayansi huyu mkuu, alimwambia, kasema, “Vema, huo basi unaweza kuzama wote?”

Akasema, “Ati unaweza? Utazama!”

⁵⁶ Kasema, “Vema, hapana shaka, huenda ikawa ni miaka mingi, mingi sana tangu sasa.”

⁵⁷ Akasema, “Inaweza ikawa ni katika dakika tano tangu sasa, ama inaweza ikawa ni miaka mitano tangu sasa.” Aliuhesabia tu miaka mitano.

⁵⁸ Lakini kwa hakika tu kama nilivyokuwa nimesimama pale chini ya Uvuvio huo, niliiweka hukumu juu ya Pwani hiyo ya Magharibi, kisha nikafuatilia papa hapa na kuzama kwa Los Angeles, umekwisha! Hiyo ni kweli. Itatukia. Lini? Sijui mimi.

⁵⁹ Lakini, loo, ni jambo gani lililotukia? Mwajua, tuna mabara sita tu sasa. Tulikuwa na saba, lile lililozama kati ya Afrika na Marekani. Loo, ni la historia, mnajua habari zake. Sasa, kama huo ukizama, basi ninawatakeni mwangalie wakati...

⁶⁰ Huu ni ujumbe niliohuburi wakati, ninaamini, Ndugu Elij’ Perry huenda alikuwa ni shemasi hapa kanisani wakati huo, kwa yote nijuayo mimi. Lakini ulisema, “Wakati utakuja...” Sikujua jambo hilo mpaka Bibi Simpson aliponiletea hayo—hayo mahubiri hivi majuzi. Nami nimeuandika kwenye kitabu kidogo, ya kwamba, “Jangwa...” ya kwamba, “Bahari itatiririka hata iingie jangwani kwa kishindo.” Hiyo ilikuwa ni miaka thelathini iliyopita.

⁶¹ Na, hakika, Bahari ya Salton ni karibu futi mia mbili chini ya usawa wa bahari, na endapo mtibuko huo mkubwa, hiyo

nchi ikimeza kuingia namna hiyo, ikiwa ni mamia ya maili mraba, mamia na mamia ya maili mraba yakizama chini ya nchi, hiyo itayarusha mawimbi ya maji mpaka Arizona. Hakika, itayarusha.

⁶² Loo, tuko katika wakati wa mwisho, saa nzuri mno, kule kuonekana kwa Bwana Yesu! Yeye alisema, “Kutakuwako na matetemeko ya nchi mahali mahali, fadhaa ya wakati, dhiki baina ya mataifa, watu wakivunjika mioyo kwa hofu.” Kasema, “Mambo haya yatakapoanza kutukia, inueni kichwa chenu, ukombozi wenu unakaribia.” Loo, jamani!

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara walizotabiri manabii;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;

Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.
(Hakikisheni kufanya hivyo!)

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inavunjika kwa hofu;
Jazweni na Roho wa Mungu, taa zenu
zitengenezwe na kusafishwa,
Angalieni juu, ukombozi wenu unakaribia!
(Hiyo ni kweli.)

Manabii wa uongo wanadanganya, Ukweli wa
Mungu wanaukana,
Ya kwamba Yesu aliye Kristo Ndiye Mungu
wetu.

⁶³ Mliona ile picha hivi majuzi, jinsi ambavyo aliigeuza picha hiyo upande mwingine? Na picha yenyewe hasa ya wale Malaika saba wakiinuliwa, ukiigeuza upande wa kulia, na hapo pana uso wa Bwana Yesu akiangalia chini duniani tena.

⁶⁴ Mnakumbuka wakati nilipohubiri *Zile Nyakati Saba Za Kanisa*, nisingeweza kufahamu ni kwa nini Yesu alisimama pale akiwa na “nyeupe” kichwani mwake mwote. Alikuwa ni kijana Mwanamume. Niliirejesha kwenye Biblia, ikasema, “Yeye alikuja kwa Mzee wa Siku, ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu.” Yesu alikuwa na umri wa miaka thelathini na mitatu na nusu tu, wakati wa kusulibishwa Kwake.

⁶⁵ Nilimpigia simu Ndugu Jack Moore, mwanatheolojia. Akasema, “Loo, Ndugu Branham, huyo ni Yesu katika hali Yake iliyotukuka.” Kasema, “Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Yeye aligeuka akawa hivyo.” Hilo lilisikika sawa kwa mwanatheolojia, bali halikuafiki, halikugonga kitu chenyewe.

⁶⁶ Nilipanda nikaenda kule na kuanza kwenye ule wakati wa kwanza wa kanisa, hapo Roho Mtakatifu akalifunua. Sasa mnalo sawa sawa kwenye *Nyakati Za Kanisa*. Nadhani vitabu hivyo vitatoka hivi karibuni sana sasa, utondoti wake wote. Nalo lilionyeshwa ya kwamba Yesu alikuwa ni Hakimu. Kuna

wigi nyeupe waliyokuwa wakivaa, wakavaa wigi na kuivaa kama hakimu, Uingereza ingali inafanya hivyo wakati ukiwa na mamlaka makuu. Na kule kuigeuza picha hiyo upande mwingine, Huyo hapo, nywele Zake nyeusi, unaweza kuona jambo hilo kando ya ndevu Zake, na amevaa hiyo wigi nyeupe. Yeye ndiye mamlaka ya mwisho, Yeye Ndiye Mamlaka ya juu kabisa. Hata Mungu alisema hivyo, Yeye Mwenyewe, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye.”

⁶⁷ Huyo hapo pamoja na hao Malaika, ule Ujumbe, ambao ulikuwa ni kule kuvunjwa mara saba kwa hiyo mihuri saba ambayo ilifunua *uzao wa nyoka* na mambo haya yote hapa. Na inaonyesha ya kwamba ndicho kifuniko Chake hasa, ni—ni Mamlaka Yake ya Juu kabisa. Yeye Ndiye Mkuu kabisa, Naye amevaa wigi, ama—ama amefunikwa. Biblia ilisema ya kwamba alibadilisha sura Yake, ama alijibadilisha Mwenyewe, *en morphe*. Neno hilo linatokana na Neno la Kiyunani, *en morphe*, ambalo linamaanisha mwigizaji wa Kiyunani ambaye anaigiza sehemu nyingi; leo hii yeye ni kitu kimoja, katika onyesho linalofuata yeye ni kitu kingine. Yeye alikuwa ni Mungu, Baba, katika onyesho moja; Mungu, Mwana, katika onyesho lingine; na halafu Mungu, Roho Mtakatifu, katika onyesho hili. Unaona? Huyo hapo, Neno Lake lingali ni Kuu kabisa. Tunaishi katika siku za mwisho.

⁶⁸ Nikirudi kutoka Afrika hivi majuzi, kidogo nilikuwa nimechoka. Unaona, ni ninii tu ni wakati wa usiku sasa kule, nawe inakubidi kugeuka. Na ndipo wakati nilipogeuka, nilirudi tena. Tulikuwa na safari nzuri sana, safari ya kuwinda, moja ya zilizo nzuri sana nilizopata kuwa nazo maishani mwangu. Halafu Billy ana baadhi ya picha, labda atapata wakati anaoweza kuzionyesha mahali fulani, na kuwaonyesha safari hiyo.

⁶⁹ Niliota ndoto. Daima ninaota kuhusu kurudi kwenye ile Kampuni ya Utumishi wa Umma, kwa namna fulani. Kwa hiyo ni—nilifikiri kwa namna fulani nilikuwa nikiizembea kazi hiyo, nilipaswa... Waliniacha nifanye nipendavyo, nami nikawazia ningeninii... Badala ya kutoka kwenda nje na kutembea kwenye nyaya za umeme ama kukusanya bili, ama chochote kile nilichopaswa kufanya, nilisema tu, “Vema, mimi ni bosi wangu mwenyewe,” nikaenda tu kuogelea. Ndipo nikafika kule chini na kuvua ninii yangu... nguo hizi, kisha nikavaa nguo zangu za kuogelea. Nilikuwa peke yangu. Ndipo nikawazia, “Aisee, hii si sawa, kampuni... Huu ni mchana, kampuni inanilipa kwa wakati huu.” Nikawaza, “Ajabu hii.” Na kisha nikawaza, “Vema, zile fedha nilizokusanya kwenye kuzunguka...” Nilikuwa na zile za doria na za mzunguko zimechanganyikana, ndipo nikasema, “Vema, pesa nilizokusanya, nimefanya jambo fulani, kurukaruka hapa; nimepoteza risiti zangu zote, na nimechanganya fedha zao

pamoja na zangu. Sasa nitajuaje ni nani aliyelipa bili?” Nikawazia, “Ni kwa sababu tu sikuwa makini!” Nikawaza, “Hilo si sawa. Kuna jambo moja tu ninaloweza kufanya, hilo ni, kurudi kwa msimamizi wangu na kumwambia.” Huyu alikuwa ni Don Willis, nikasema, “Don, nilipoteza zile risiti. Sasa hizi hapa pesa zote nilizo nazo, na hizi hapa pesa zao, pamoja. Nitaziacha hapa kwa keshia. Nao watu, watakapokuja, watakuwa na risiti kwamba nilipokea bili zao.”

⁷⁰ Huenda ikawa wapo watu wanaoketi hapa ambao ni—ni . . . ninajua wapo. Ambao nilizichukua kutoka kwao katika—katika siku hizo, nami ningeninii . . . nami ningetwa risiti. Mwajua, ilikuwa ni asilimia kumi tu kama ukiacha bili yako ipite. Na labda, dola moja na nusu, itakuwa ni senti kumi na tano zaidi. Wengi wa watu hao waliishi . . . Tulipenda tu kuketi pamoja na kuzungumza, nao wangeachilia bili zao tu zipite, nami ninakuja kuzungumza nao kidogo. Kutoa senti kumi na tano, mwajua, kuketi tu chini na kuzungumza kidogo, na kukusanya bili zao. Kwa hiyo mambo yakaharibika sana, na ikawa kuna bili nyingi kupita kiasi ambazo nisingeweza kuzikusanya.

⁷¹ Vema, nilidhani hivyo ndivyo tu ningaliweza kufanya hilo. Ndipo nikaamka.

⁷² Mahali tunapoishi, Dada Larson, sidhani kama yupo hapa, amekuwa mwema sana kwetu; na yeye hapendi niseme hivyo. Lakini yeye ni mama mzuri sana, nasi tumekuwa tukiishi katika vyumba vyake. Ana fleti mbili, fleti ndogo pamoja, tulizikodi zote mbili. Nami na mke wangu tunalala hapa katika—katika fleti ambako kwa namna fulani ninawapokea watu niwezapo, na kuna vitanda vidogo vichache vya watu wawili mle ndani.

⁷³ Niliamka. Hakuwa ameamka bado. Na baada ya kitambo kidogo, akaamka. Nami nikampungia mkono, naye akaangalia nyuma na kupepesa macho yake mara kadhaa. Nikasema, “Ulilala vizuri?”

Akasema, “Hapana.”

⁷⁴ Nami nikasema, “Nilikuwa na ndoto mbaya sana. Nilikuwa nimerudi kwenye ile Kampuni ya Utumishi wa Umma tena.” Nikasema, “Nimefanya nini?”

⁷⁵ Ninakumbuka, kama mvulana mdogo, ama kijana, nilitembea kwenye nyaya hizo zote huko Salem, Indiana, tofauti . . . Ningeingia, ninanunua ki—kiamshakinywa, labda bakuli ya uji wa shayiri. Katika jua hilo lenye joto na kila kitu, nao ungenichefua tu, kula kiamshakinywa. Ningetumia senti kumi, kwenye fedha zangu za kichele. Msimamizi angeshuka aje na kusema, kasema, “Unajua walichosema m—mkutanoni? ‘Ni nani huyo baradhuli ambaye angetumia senti kumi, kwa kiamshakinywa?’” Kasema, “Unapaswa angalau kutumia senti hamsini.” Sasa, nyote mnajua, senti hamsini ilikuwa ni kiamshakinywa kingi siku hizo.

Nami nikasema, “Vema, sili kiasi hicho.”

Akasema, “Vema, hao wengine wanatumia senti hamsini. Unapaswa kutumia senti hamsini.”

Nikasema, “Vema, sizitumii.”

Kasema, “Zitumie, haidhuru.” Huyu alikuwa ni msimamizi wangu.

⁷⁶ Vema, nikawaza, “Vema, nifanye nini? Sina budi kutoza senti hamsini, kisha nile senti kumi.” Kwa hiyo ningetoka kwenda mtaani na kuwakusanya watoto wadogo ambao hawakuwa na kiamshakinywa, na kuwanunulia kiamshakinywa cha gharama ya senti arobaini.

Kwa hiyo basi nikafikiria, “Vema, ni kitu gani ningeweza kuninii . . . Labda hilo ndilo kosa amenipata nalo.”

⁷⁷ Nami nakumbuka, hapa si muda mrefu uliopita, walikuja huku kufanya doria, wakabomoa kile kitalu cha nyuma pale, na kusema, “Lipa bili yako.” Unajua wana haki za doria, bali inawabidi kulipia uharibifu.

⁷⁸ Niliandika barua nikasema, “Hamna deni lolote.” Nikawaza, “Hiyo ingelipia zile senti arobaini. Labda nimetumia dola ishirini ama thelathini kwenye wakati huo, nikiwapa watoto. Labda hiyo italipia.” Nikaendelea kuota.

⁷⁹ Halafu nilikuwa na mti mkubwa huko nje, watoto walicheza chini yake, na doria . . . Sasa wanafanya doria kwa helikopta. Na kwa hiyo aliingia na kusema, “Billy, vipi kuhusu kuukata ule mti?”

⁸⁰ Nikasema, “La, usiukate. Tutaupogoa.” Nikasema, “Mimi na Ndugu Wood tutaupogoa.”

Kasema, “Vema, nitamtuma mtu aje hapa na kuupogoa.”

Nikasema, “Sasa, usiukate.”

Akasema, “Sitaukata.”

⁸¹ Nikaenda safari. Niliporudi, ulikuwa umekakwa mpaka chini. Ndipo nikaandika mashtaka, mnaona. Nikasema, “Vema, Bwana, hii italipia jambo lile kabisa, najua.” Kwa hiyo nikafutulia hiyo mbali, hiyo ilikuwa ni sawa, nikaiachilia tu. Vema, ningali niliota hiyo.

⁸² Nilipoamka hivi majuzi asubuhi, nilisema, “Vema . . .” Jambo la kwanza tunalofanya asubuhi tunapoamka, ni kuomba pamoja, halafu tunaomba tunapoenda kulala usiku. Halafu basi wakati alipoenda huko kuwapa watoto kiamshakinywa, nilianza kuomba. Nikasema, “Bwana, hapana shaka nilikuwa jamaa mbaya sana. Nimefanya nini maishani, hata si—siwezi kuisahau ile Kampuni ya Utumishi wa Umma.”

⁸³ Nikaingia ndani nikaoga, kisha nikatoka nje. Na kitu fulani kilionekana kuniambia, “Labda ninazembea kwenye kazi *Yake*.”

Nikafikiri, “Hii hapa kadiri ya miaka mitano ambapo sijafanya kitu, ninamngojea tu.”

⁸⁴ Nikiwa nimesimama pale hivi majuzi. Walitujengea nyumba mpya kule juu, na Ndugu Mosley akashuka akaja, alikuwa akizungumza habari zake. Nikasema, “Hiyo ni zawadi ndogo tu kutoka kwa Baba yangu.” Naye akaanza kulia. Nikasema, “Unaona, Yeye alisema, ‘Kama mtaacha makazi yenu, nyumba, mashamba, baba, mama, nitawapa nyumba, mashamba, baba, mama, na mara mia katika maisha haya, na Uzima wa Milele ujao.’” Nikasema, “Mnaona, ilinibidi kuiacha maskani ninayoipenda sana. Nyumba yangu ambayo Mungu alinipa huko, ilinibidi niiache. Amenirudishia tu hii.” Nikasema, “Yeye ni mwema sana, mnaona.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ndipo akaanza kulia.

⁸⁵ Vema, ni—nikasema, “Ilinibidi kuja huku nje na kujitenga, kuja kwenye jangwa hili.” Ndipo nikawaza, “Sijui ni kwa nini Mungu angenileta kwenye jangwa, huku nje ambako hakuna kitu ila nge na wanyama wakali kama vile Gila.”

⁸⁶ Si jangwa tu, ni joto, bali kiroho ni jangwa. Loo, jamani! Hakuna maisha ya kiroho hata kidogo, makanisani, wanapinga... Mbona, hujapata kuona kitu kama hicho maishani mwako! Hata hatuna kanisa la kuhudhuria, wala chochote kile. Na halafu wakati... Watu karibu wanaangamia, kiroho. Ninaliona katika watu wanaokuja huko, kuona tofauti kati yao, nikiangalia.

⁸⁷ Na kwa hiyo unakaa chini ya Roho wa Mungu, na maisha yako yanakuwa matamu, mororo, kama vile maji yanavyoleta nyasi hii na chipukizi nyororo. Kama... nyasi hii, huku Arizona, isingekua; miti hii ingekuwa ni mipungate, hayo majani yanajikunja tu na kufanya miiba. Hivyo ndivyo ilivyo wakati mnapokuwa wakavu kanisani, kila mtu anamchoma mwenzake, unajua. Na, unaona, huna budi kupata maji matamu ya mvua kukulainisha, na kufanya majani na kivuli kwa ajili ya msafiri apitaye hapo.

⁸⁸ Na basi kitu fulani kikaniambia, “Labda unazembea katika kazi Ya Mungu.” Kwa hiyo, nikaomba nipate ono.

⁸⁹ Na Meda ndiyo kwanza aninunulie Biblia mpya; na Ndugu—Ndugu Brown, kutoka huko Ohio, akaninunulia Biblia mpya; wote wawili kwa wakati ule ule wa Krismasi. Nilienda nikachukua moja ya Biblia hizo mpya. Nikasema, “Bwana, katika siku zilizopita, Wewe ulikuwa na Urimu na Thumimu.”

⁹⁰ Sasa sikilizeni, hebu niseme jambo hili. Hakika, wao hawaninii... huu, hawaurekodi mkutano huu, ndiyo sababu ninauli... ninasema jambo hili. Hebu niseme, usifanye jambo hili. Si jambo jema.

⁹¹ Lakini nilisema, “Bwana, ilikuwa kwamba, wakati mwotaji alipoota ndoto, kwamba waliipeleka kwenye Urimu na

Thumimu, na kuisimulia. Na kama ninii—kama Urimu na Thumimu iliakisi hizo nuru, Nuru ya kimbinguni, hiyo ndoto ilikuwa ni ya kweli.” Nikasema, “Lakini ukuhani huo na Urimu na Thumimu hiyo imeondolewa. Biblia Yako ndiyo Urimu na Thumimu sasa; Bwana, nijalie nisifanye jambo hili tena. Lakini nimekusihi na kukuomba Wewe, unipe ono, sema nami ni kwa nini ninaota ndoto hizi. Na nimefanya nini? Kama nimeudhi, kama nimefanya lolote kwa mtu yeyote ulimwenguni, nijalie kujua. Nita—nita—nitaenda kulisahihisha. Kama ninaiwia Kampuni ya Utumishi wa Umma, kama nimewakosea ama kumkosea mtu yeyote mwingine, kama nimekukosea Wewe, nijalie nijue. Na—nataka kulisahihisha.”

⁹² Hebu tulisahihishe, sasa. Usingoje mpaka baada ya kitambo kidogo, huenda ikachelewa sana. Hebu tulifanye sasa.

⁹³ Ndipo nikasema, “Hakika, kuna jambo fulani katika Neno hili la Mungu, tangu Mwanzo hadi Ufunuo, ambalo mtu fulani humo ndani ambaye Wewe ulimshughulikia, angekuwa kwenye msingi ule ule ambao swali langu lingehusiana nao. Kama mtu fulani amefanya jambo fulani, na—na Wewe ukamfuatilia kulihusu, basi hebu nifungue mahali hapo katika Biblia. Na endapo mtu fulani, lolote ambalo walifanya, litaegemea upande wangu. Ambapo nimekosea, ama jambo fulani unalonitaka nifanye, ama sijalifanya, jalia nione mtu fulani katika Biblia wa jinsi hiyo.”

⁹⁴ Ndipo nikafumba macho yangu, nikaiacha tu Biblia ijifungue, nikaweka kidole changu kwenye Andiko, Mwanzo 24:7. Elieza, mtumishi mwaminifu wa Ibrahimu, aliye mtumishi kielelezo katika Biblia, akitumwa kwenda kumtafutia Isaka Bibi-arusi. Ubaridi ukanivamia. Hakika, hiyo ndiyo ninii yangu...hiyo inaambatana kabisa na Ujumbe wangu wote, kumvuta Bibi-arusi atoke.

⁹⁵ Akasema, “Apa ya kwamba hutamchukua bibi-arusi kutoka kwa hawa, bali uende kwa watu wangu mwenyewe.”

Akasema, “Vipi kama mwanamke huyo hataambatana na mimi?”

⁹⁶ Kasema, “Basi uko huru na kiapo hiki.” Akasema, “Na Mungu wa Mbinguni atamtuma Malaika Wake mbele zako, kukuongoza.” Akaondoka moja kwa moja na akaanza kuomba, ndipo akakutana na mrembo Rebeka ambaye alifanyika bibi-arusi wa Isaka.

⁹⁷ Ujumbe mkamilifu tu, kurudi kwenye Neno, “Nenda ukamlete Bibi-arusi huyo!” Hilo ni jukumu. Hiyo ndiyo sababu ya mimi kuwapo hapa. Hilo ndilo ninalojaribu kufanya, ni kumwita Bibi-arusi atoke.

⁹⁸ Kumbukeni huko California kule, yale mahojiano ya Bibi-arusi, kule kuonyeshwa kabla, nilikuwa nako hapa. Jinsi ambavyo huyo Bibi-arusi alijitokeza kwanza, na nikamwona

akipita. Kisha huyu hapa Bi Marekani anakuja, Bi Asia, na wote wale, loo, kitu kilichoonekana ni kibaya kuliko vyote! Na ndipo Bibi-arusi yule yule akapitia pale tena. Mmoja wao akatoka kwenye mstari, nami nilikuwa nikimrudisha kwenye mstari; wawili wao, ndivyo ilivyokuwa. Na hivyo ndivyo nilivyopaswa kufanya, kumweka Bibi-arusi huyo kwenye mstari, nimtafute mtu huyo.

⁹⁹ Nikasema, “Mungu, ninarudi nyumbani, nifanye upya nadhiri zangu tena, na kuanza upya.” Kwa hiyo hilo ndilo tunalopanga kufanya, hiyo ndiyo sababu nipo hapa.

¹⁰⁰ Nafikiri lingekuwa ni jambo jema kama tungelifanya jambo hili, tungeanzia kwenye tarehe kumi na nane, juma lijalo, Jumapili ijayo asubuhi, Jumapili ijayo usiku; Jumapili inayofuata, na Jumapili inayofuata. Ni wangapi wanaofikiri hilo lingekuwa ni jambo jema? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Asanteni.

¹⁰¹ Sasa ninawatakeni mnifanyie jambo fulani. Kama mmewajulisha watu wowote kwamba ku—kutakuwako na mkutano kwenye tarehe ishirini na nane, naomba muwatangazie tena, ya kwamba tusingeweza kuufanya. Waambieni, waandikieni barua, ama kitu kama hicho. Hatutaki watu waje na kuudhika, bali tusingepata jumba la mkutano.

¹⁰² Mnaona, tusingelipata. Na kwa hiyo kwa sababu mkutano wa mwisho nafikiri tulikuwa na watu wengi sana kule, na kila kitu, walinii tu. . . Mnajua jinsi umma ulivyo, na wao. . . Vema, tunaishi tu katika siku za mwisho, hivyo tu. Nao wanadai ya kwamba hao watu wanakuja na kusumbua shule, nao walikuwa huko mapema sana, na walifanya *hili*, ama *lile*, ama jambo jingine, na mahali hapo palijaa kupita kiasi, na zimamoto anafanya *hili* na *lile*. Na, vema, mwajua.

¹⁰³ Kwa hiyo tutapanga hivyo Vitasa na hizo Baragumu, ninataka kuziweka ndani. Niliwaambia nitaziweka. Zinakuja chini ya kitu kingine. Vivyo hivyo na Vitasa vinakuja, kule kupigwa kwa baragumu; bali tunataka kulipitia somo hilo zima, na kulileta, kuliunganisha pamoja.

¹⁰⁴ Ni wangapi wamesoma chochote cha Ndugu Vayle, juu ya kukihariri hicho tena, na kukitengeneza na kunitilia hicho sarufi? Mmesoma sehemu yoyote yake? Mmesoma, wawili ama watatu wenu. Nafikiri umefanya kazi nzuri sana, Ndugu Vayle, kazi nzuri sana! Wewe, nafikiri Dada Vayle aliifanya; nawe ulikiandika tu. Yeye—yeye alikuwa ninii. . . Mnaona, mimi sikuzote siwapingi wanawake, sivyo, Dada Vayle?

¹⁰⁵ Kwa hiyo sasa hebu, kwa dakika kumi na tano zifuatazo, ishirini, tusome Andiko hapa.

¹⁰⁶ Nami nina kitabu kidogo hapa. Nilimwambia, ninaamini, alikuwa ni Ndugu Vayle, ama, alikuwa ni nani, ama ninaamini

ilikuwa ni Roy Borders. Ndugu Vayle aliniletea kitabu hicho. Ninataka kuandika kitabu kidogo cha kiada.

¹⁰⁷ Lakini kama mtu yeyote aliangalia kile ninachoita mihtasari! Kama vile ningetaka kuhubiri juu ya Nyota ya Asubuhi, nitachora nyota. Na kama nikitaka kuhubiri kitu fulani kuhusu...Ninaviandika vyote katika ishara hapa, mikwaruzo, hakuna mtu anayeweza kujua kamwe kwamba ilikuwa ni nini. Ninapokuwa nje, nami niwazie juu ya kitu chochote, inanibidi, juu ya kuendesha gari barabarani, wakati mwingine gari likirukaruka, nami nitaandika *hili* chini upesi, na kusema *hili* na *lile*, na kufanya ishara ndogondogo, na msalaba na madaraja, na—na kila namna ya vitu. Kama vile nikitaka kuhubiri juu ya kushuka kwa ile Nyota; basi nitaweka piramidi, niichore hapa na kuweka ile nyota ya Daudi yenye ncha tano ikishuka juu yake. Nami ninajua mahali ninapoelekea kwenye Maandiko namna hiyo; naye Musa, jambo fulani alilofanya. Ninafanya tu vitu kama, vinjia vidogo kama vya batamzinga.

¹⁰⁸ Ninazo kadhaa hapa ndani. Nami niliwazia, asubuhi ya leo, huko nyuma wakati nilipowazia nitahubiri juu ya somo hili kwa dakika chache hapa, juu ya mhtasari, labda itanichukua dakika ishirini.

¹⁰⁹ Na halafu basi sitachukua ibada ya Ndugu Neville usiku wa leo. Ni—ni—nitapumzika usiku wa leo, nimsikilize.

¹¹⁰ Halafu basi, Bwana akipenda, Jumapili ijayo asubuhi tutaanza ibada. Nanyi nyote mnisaidie, nasi tutaomba, kwa maana lilikuwa moyoni mwangu kujaribu...Wao walisema, “Vema, tungeenda Louisville ama tungeshuka twende huko New Albany.” Lakini mkutano huo ulipaswa kuwa ni wa Jeffersonville. Nitaenda Louisville na New Albany, katika nyakati tofauti, lakini huu unapaswa kuwa hapa Jeffersonville.

¹¹¹ Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja wakati tumekuwa...Nimekuwa nikizungumza nanyi hapa kwa karibu dakika thelathini. Hebu na tuseme Naye kwa muda kidogo.

¹¹² Bwana Yesu, sisi—sisi kwa hakika ni watu waliobarikiwa, kupita mawazo yetu, kupita ufahamu wetu. Kwa kuwa, kama kungalikuwako na mtu mashuhuri miongoni mwetu, kama vile wajumbe kutoka nchi nyingine, ama mwanadiplomasia fulani, tungefikiri lilikuwa ni jambo kuu kuwa na mtu mashuhuri kama huyo miongoni mwetu. Lakini leo hii tuna Mungu wa Mbinguni, si miongoni mwetu tu, bali ndani yetu, akiishi, akiishi Maisha Yake kupitia sisi. Nasi tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili, Bwana! Limepita ufahamu wetu, bila shaka.

¹¹³ Lakini sasa tukinena juu ya ibada hizi, na kwenda Afrika, na mambo ambayo tumejaribu kuyaandaa kwa siku hizi chache hapa Indiana. Na kwa njia moja ama nyingine, Bwana, huenda ikawa Wewe unatuelekeza kwenye lile hema, kulitimiza lile ono. Kwa hiyo mapenzi Yako yafanyike, tumeyakabidhi hivi, kadiri

tujuavyo sisi. Kwa hiyo tunaomba, Bwana, kama kuna kitu chochote kinyume na mapenzi Yako, utatujulisha hicho, tupate kujua kufanya mapenzi Yako makamilifu.

¹¹⁴ Sasa tubariki katika dakika hizi chache zifuatazo. Nena nasi kupitia Neno Lako, Bwana, kwa kuwa Neno Lako ni Kweli. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Hebu na tufungue katika Biblia, katika Marko, mlango wa 8.

¹¹⁵ Huwa mnaondoka wakati gani kwa kawaida, saa sita? [Mtu fulani anasema, “Kama saa sita.”—Mh.] Vema. Sasa, sasa Ujumbe mfupi tu hapa ambao ninaweza kuwazungumzia kuhusu Neno, baada ya kushuhudia kuhusu mambo ya kule, na kadhalika.

¹¹⁶ Marko, mlango wa 8, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 34, hadi cha 38, tukichukua cha 38, mwisho wa mlango huo. Ninapenda kusoma yale Yeye aliyosema, maana ninajua ya kwamba hayo ni kweli. Sasa sisi . . .

Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuata.

Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, . . . mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha.

Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?

Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?

Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.

¹¹⁷ Ninataka kuchukua kifungu kidogo kutoka hapo, kama kingeitwa hicho, kinachoitwa: *Kuonea Haya*. Unajua, ninapenda jambo hilo. “Kila mtu atakayenionea haya Mimi na maneno Yangu, nitamwonea haya.”

¹¹⁸ Sasa, neno *kuona haya* lingeweza pia kutafsiriwa “kutahayarishwa.” Unajua, kitu fulani ambacho unaninii . . . Unakabiliwa na jambo ambalo unalionea aibu, kuona haya.

¹¹⁹ Hilo, jambo lingine kuonea haya hufanya, huonyesha ya kwamba huna hakika na jambo unalonena habari zake. Kama unajua lile unalozungumzia, na una hakika ya kwamba unajua lile unalozungumzia, unaweza kumwambia mtu yeyote jambo hilo; huoni haya. Lakini kama ukijisikia kunyamazishwa, hufai, inaonyesha huna hakika.

120 Unaona kuna mengi sana ya hayo siku hizi, hasa juu ya somo ninalozungumzia, “*kulionea Neno haya*.” Sasa, Yeye na Neno ni yeye yule.

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, . . . Yeye yule jana, leo, na hata milele!

121 Kwa hiyo, “Kila mtu anayenionea haya Mimi na Neno Langu,” Naye na Neno Lake ni Mmoja, kwa hiyo kulionea haya Neno Lake katika kizazi hiki cha sasa cha dhambi, “Nitamwonea haya.”

122 Sasa tunaona siku hizi, kama mtu fulani akisema, “Hivi—hivi wewe ni Mkristo?” Ni jambo linalopendwa sana na watu, kusema, “Loo, Mimi ni Mkristo!” Unaona?

123 “Lakini unaliadini Neno la Mungu, ambapo lilisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio?’”

124 “Loo!” Hata nyuso za wahudumu zitatahayari. Unaona?

125 Je! unaonea haya, tuseme, uponyaji wa Kiungu? Unaonea haya Injili yote? Unalionea haya tukio lako la kipentekoste? Huko ni kulionea haya Neno Lake. Hilo ni Neno Lake lililofanyika mwili ndani yako.

126 Kwa hiyo, Neno Lake halina budi kujiishi Lenyewe kwa kila kizazi. Lilijiishi Lenyewe katika siku za Musa. Kwa sababu, katika siku hiyo, Biblia ilisema, katika Waebrania, mlango wa 1, “Mungu, alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi.”

127 Na hao manabii! Kanisa lilivurugika kabisa hivi kwamba wakati. . . Hao manabii, hao wajumbe wajasiri wa Mungu, walikuja bila kanisa, bila dhehebu, bila shirika, bila chochote; wakawaasi wafalme, milki za wafalme, makanisa, na kila kitu. Wakati makuhani walipoletwa mbele ya. . . Walipoletwa mbele ya makuhani, hawakuona haya, kwa sababu walikuwa na moja kwa moja BWANA ASEMA HIVI.

128 Kama ukiangalia, nabii, katika maana moja ya neno, katika Agano la Kale, wakati aliposema BWANA ASEMA HIVI, sasa mwangalie, anaingia moja kwa moja katika msemu wa kuchukua mahali pa Mungu. Unaona, wakati alipoweka mbele yake, BWANA ASEMA HIVI, aliingia moja kwa moja kwa Mungu, na kutenda kama Mungu. Ndipo akatoa Ujumbe wake, ambao ulikuwa ni Mungu akinena kupitia kwake, “BWANA ASEMA HIVI!”

129 Ninafikiria kuhusu manabii wa kale, walipokuja na Ujumbe huo, nao ukawatahayarisha wafalme, na kuwatia watu wasiwasi. Makuhani, hata, nao wangekuwa na wasiwasi, kwa sababu walipaswa kuwa ni viongozi, watu wa kidini, na wakati

waliponinii . . . Neno lilipowajia kwa njia hiyo, liliwaanika wazi, nao wakatahayari, ama wakaona haya.

¹³⁰ Na mara nyingi tunaona ya kwamba, si wengi, mara nyingi sana siku hizi! Huyu mtu, unasema, “Mimi ni Mkristo!”

“Je! umempokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?”

“Loo! A-ha!” Unaona, wa—wao wanatahayarishwa na jambo Hilo.

¹³¹ Mtu fulani akisema, “Je! wewe ni mfuasi wa lile kundi pale juu linalopiga makelele hayo yote pale, na upuuzi huo wote wa uponyaji wa Kiungu?” Mara nyingi, Wakristo wanaghairi.

¹³² Wanataka kutangaza, kama—kama wana dhehebu, sasa, “Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mlutheri.” Hawalionei haya hilo.

¹³³ Lakini inapofikia kuwa Mkristo ambaye anaweza kulichukua Neno la Mungu jinsi tu lilivyo, basi wana—wana—wanaona haya. “Mimi si mfuasi wa dhehebu lolote,” unaona, wao, wana—wanaona haya kusema hilo. Hawana budi kuwa kama walimwengu wengine, wanaowakilishwa na dhehebu fulani.

¹³⁴ Sasa, hilo limefikia hapo tu hivi miaka ya karibuni. Katika siku za Luther, kujitambulisha kama Mlutheri ama mfuasi wa Luther, vema, karibu ilimaanisha kuuawa na kanisa Katoliki. Katika Siku za Wesley, kujua ya kwamba ulikuwa umelikataa kanisa la Kianglikana, ilikuwa karibu ni hukumu ya mauti kwa Waanglikana, kutangaza ya kwamba ulikuwa Mmethodisti. Katika siku za Pentekoste, ilikuwa karibu, ni aibu, kusema ya kwamba wewe ulikuwa—kwamba wewe ulikuwa u mpentekoste, kwa sababu upesi ulihesabiwa kama mtakatifu anayejifingirisha, ama—ama mnenaji fulani kwa lugha, ama kitu kama hicho. Sasa wao waliunda dhehebu na wakaungana na hao wengine wa kundi hilo.

¹³⁵ Sasa wakati wa kuitwa utoke unapokuja, kwamba wewe si mfuasi wa lolote la hayo! Ni jambo linalopendwa sana na watu kusema, “Mimi ni Mpentekoste.” Ni jambo linalopendwa sana na watu kusema, “Mimi ni Mpresbiteri. Mlutheri.” Lakini vipi wakati inapofikia wakati ambapo itakubidi kujitokeza nje na kulitetea Neno, “Mimi si mfuasi wa lolote la hayo”? Hilo, hilo lilitahayarisha.

¹³⁶ Yesu alisema, “Sasa, kama ukinionea haya, basi nitakuonea haya.” Ni kwa nini akuonea haya? Ni kwa sababu unadai kuwa ni Wake, wakati hutamfuata.

¹³⁷ Vipi kama nilisema, “Mvulana huyu mdogo, yeye—yeye ni mwanangu”; ageuke na kusema, “Ati nani, ati mimi ni mwanao? Kwani unafikiri mimi ni nani!” Ingenitahayarisha. Ingekutahayarisha, kwa mwanao.

¹³⁸ Na hiyo ndiyo njia inayoitwa Ukristo siku hizi. Ukilipa jina la dhehebu, sawa, wanakubali ubaba wa dhehebu. Lakini inapofikia kuukubali ubaba wa Neno la Mungu, Kristo, la, wanatahayarika. Hawataki kusema, “Naam, nimenena kwa lugha. Naam, nimeona maono. Naam, ninaamini katika uponyaji wa Kiungu. Naam, ninamsifu Bwana. Niko huru na madhehebu yote, sisujudii yoyote ya hayo. Mimi ni mtumishi wa Kristo.” Loo, jamani, hilo lingewararua tu vipande-vipande.

¹³⁹ Hivi majuzi usiku, mhubiri mashuhuri alikuja miongoni mwa Wafanya Biashara wa Full Gospel huko Chicago.

¹⁴⁰ Hebu nisimame hapa kidogo, kusema jambo hili. Samahani. Lakini mara nyingi unafikiri, nami pia ninafikiri, ya kwamba kile tunachonena habari zake, Kweli ya Biblia, watu hawaielewi. Lakini, inawaelea. Wakati mwingine wataungana moja kwa moja kuipinga, bali kwa kweli hawamaanishi kufanya hivyo. Wanajaribu kuona msimamo wako.

¹⁴¹ Kama vile hadithi ilivyosimuliwa juu ya kundi la walevi, wakibishana kwamba hakukuwako na kitu kama Ukristo. Mtu mmoja akasema, “Ninajua mahali mmoja alipo, huyo ni mke wangu.”

Kasema, “Vema, si—siamini jambo hilo.”

Kasema, “Hima twende, tutaninii. . . hebu sisi sote tufanye kana kwamba tumelewa sana.”

¹⁴² Wakapanda wakaenda huko nyumbani, na wakafanya kila kitu walichoweza. Na—na kuwaambia wawapikie mayai, na ndipo akayatupa sakafuni, na kusema, “Unajua vema zaidi kuliko kuyapika mayai yangu namna hiyo!” Wakifanya vurugu nyumbani. Ndipo wakaingia kwenye chumba hicho kine, wakajibwaga kitini. Wakamsikia mtu fulani huko akifagia, hasemi neno, akisema, akijiimbia wimbo mdogo.

Hivi sharti Yesu aubebe msalaba peke yake,

Na ulimwengu wote uwe huru?

Kuna msalaba kwa kila mtu,

Na kuna msalaba kwa ajili yangu.

Basi msalaba huu uliowekwa wakfu
nitaubeba,

Mpaka mauti itakaponiweka huru,

Kisha niende nyumbani kuvaa taji.

¹⁴³ Huyu mlevi mmoja mzee akasema, “Niliwaambiaje?” Kasema, “Yeye ni Mkristo!” Mnaona, walikuwa tu wakimjaribu. Na wakati mwingine ulimwengu, nimegundua, hukujaribu.

¹⁴⁴ Kwa hiyo sikudhani jambo hili lingetukia, lakini Jumamosi iliyopita usiku, ninaamini ndiyo, ama Jumapili usiku, yule mnenaji mashuhuri. . . sijazoea kuyataja majina ya watu. Lakini yeye anajaribu, akitenda kazi kinyume kabisa. Ninajaribu kuyaweka makanisa hayo mbali na ule mwenendo wa

ekumenia, na mtu huyu anajaribu kuwaingiza mle. Kwa hiyo, alikuwa akihubiria Wafanya Biashara Wakristo. Ambapo, nilikuwa nimekusudiwa kuwa na mkutano Chicago, nami nikawaza ngingekuwa Afrika wakati huo, kwa hiyo nisingeweza kuuchukua. Mtu huyu akasema, alisimama pale na kusema, “Uamsho ulio mkuu kuliko yote, kitu kilicho kikuu kuliko vyote duniani wakati huu, kilichopata kuwapo; makanisa yote yanarudi kwenye kanisa Katoliki, katika mwenendo wa ekumenia, nao Wakatoliki watampokea Roho Mtakatifu.” Ni mtego wa jinsi gani wa Ibilisi!

¹⁴⁵ Na kiongozi huyu, Ndugu Shakarian, rais wa Wafanya Biashara wa Kimataifa, akasimama na kusema, baada ya mtu huyo kuketi chini, kasema, “Hivyo sivyo tulivyolisikia jambo hilo.” Kasema, “Ndugu Branham ametwambia, ya kwamba, ‘Mwenendo huu wa ekumenia utawapeleka wote kwenye alama ya mnyama.’” Na mtu huyo ameketi jukwaani. Kasema, “Utalekeza kwenye alama ya mnyama.” Kisha kasema, “Tunashawishika kuamini yale asemayo ni Kweli.” [Mtu fulani katika kusanyiko anasema, “Amina! Vivyo hivyo na sisi pia!”—Mh.] Naye akasema, “Ni wangapi wenu wangetaka kumsikia Ndugu Branham akija na kuwapa ukweli wake? Inueni.” Na kulikuwa na watu elfu tano na kitu. Walipiga makelele kwa nguvu na kulia, nije tu kwa siku moja, siku moja.

¹⁴⁶ Ndugu Carl Williams akanipigia simu, kasema, “Ndugu Branham, jamani, nilipitia katika umati huo,” kasema, “walikuwa na mafungu ya noti za dola mia moja yaliyowekwa mikononi mwangu, kukununulia tiketi ya ndege ya kuja huku, na kurudi.” Mnaona, kwa siku moja tu!

¹⁴⁷ Mnaona, watu hao, hilo Neno linaingia ndani ambapo wakati mwingine hatujui jambo hilo. Mnaona? Lakini, mnaona, wakati unaponinii kweli. . . Haidhuru ulimwengu unalipinga jinsi gani, madhehebu yanalipinga kiasi gani, Mungu analithibitisha kwamba ni Kweli. Hatimaye wakati ile saa kuu itakapofika, mambo yatatukia ambayo labda hatukuyawazia.

¹⁴⁸ Naam, inaonyesha huna hakika, kama unatahayarika, kwa hiyo ni afadhali usilijadili jambo hilo. Kama utalionea haya, usingetaka kulijadili, utajizuia.

¹⁴⁹ Lakini anawezaje mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, anawezaje mtu aliyejazwa na Nguvu za Mungu, na upendo wa Mungu moyoni mwake, kuzungumza na mtu kwa dakika chache na asitaje kitu fulani kuhusu huo upendo ulio moyoni mwake? Unaona, kuna kitu fulani ambacho hu—hutukia; huwezi kufanya jambo hilo.

¹⁵⁰ Hii ni, haina budi kuwa ni siku iliyo ya uovu ambayo Yesu alikuwa akinena habari zake. Watu wanalionea haya Neno na Roho wa Mungu anayetenda kazi ndani yao. Lakini wakati Kweli

inapofanywa dhahiri kwa watu, ni Mungu basi, Mwenyewe, akijifunua Mwenyewe kwa Neno.

¹⁵¹ Sasa, mtu yeyote anaweza kufanya madai ya aina yoyote. Nasi tumekuwa na jambo hilo katika siku hizi, ambapo kumekuwako na madai mengi yaliyodaiwa, hata imekuwa ni jambo la kuchukiza sana. Lakini, unaona, kama kuna Kweli, haina budi kuwa ni kwa Neno. Kwa sababu, wanasema walikuwa na mambo ya kila namna, ya mafuta yakitiririka kupitia kwa watu, na damu kutoka mikoni mwao, na wanawake nyuma yao katika damu hii, na ikitiririka kwenye viatu vyao, na kuinua viatu vyao na kumwaga mafuta, na vyura wakiruka na kutoka na kurukaruka jukwaani, na kila namna ya mambo kama hayo. Hakuna upuuzi kama huo katika Biblia. Hakuna ahadi ya kitu kama hicho, katika Biblia. Ila tu, ilisema, “Katika siku za mwisho, roho hiyo ingefanana sana ingewapoteza walio Wateule kama yamkini.” Lakini hakuna Maandiko kwa hayo.

¹⁵² Lakini inapofikia Neno la Mungu halisi, lisiloghoshiwa, lililothibitishwa na Mungu, inaonekana kulitahayarisha hata kundi hilo lingine, lililovuka mpaka. Mnaona, kuna kutahayari kulihusu.

¹⁵³ Lakini ni halisi kwa mwanamume ama mwanamke, mvulana ama msichana, ambaye kweli ni Mkristo halisi. Wakati Mungu alipoitoa ahadi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, nawe unampokea Huyu, kuna Kitu fulani kinachotulia ndani yako, ambacho hakuna kitu kinachoweza kupachukua mahali pake. Mtu anapokutana na Mungu; si katika kuuchochea mhemko, shauku fulani, ama fundisho fulani la kidini, katekismo fulani ama kanuni ya imani, ama fundisho la sharti ambalo amelikubali kwa ajili ya kuji—kujifariji, lakini wakati kweli inapofikia mahali kama vile Musa alivyopafikia, upande wa nyuma ya jangwa, akutane uso kwa uso na Mwenyezi Mungu, nawe unaiona hiyo Sauti ikisema nawe, imeambatana kabisa na Neno na ahadi ya wakati huo, kuna kitu inachokufanyia! Unaona, huionei haya, inakufanyia kitu fulani. Sasa, hebu tuangalie sasa, kwa dakika kumi na tano tu zifuatazo.

¹⁵⁴ Kuna watu wanaopokea tukio kama hilo. Na kama ninavyosema nanyi leo, sio kama kanisa ama dhehebu, ninasema nanyi kama mtu binafsi; sio eti kwa sababu unakuja hapa kwenye maskani hii, kwa sababu ninakupenda nawe unanipenda, sio kwa sababu ya jambo hilo. Hebu ninene nawe kama mwanadamu anayekufa, ya kwamba siku moja huna budi kufikia mwisho wa maisha haya. Na huenda nisiwepo, na mhubiri mwingine huenda asiwepo. Lakini kuna Mmoja tu anayeweza kukutana nawe kule, na huyo ni Mungu. Na wewe—wewe lisikilize, na sio kama “mke wangu ni Mkristo mzuri” ama—ama “mume wangu ni Mkristo mzuri,” bali “Je! niko sawa na Mungu? Je! nimekutana na Mungu namna hiyo?” Si kwa sababu “mchungaji wangu alikutana na Mungu,” ama kwa

sababu “shemasi wangu alikutana na Mungu,” lakini, “Je! mimi nimekutana Naye?” Si kwa sababu “nilipaza sauti,” si kwa sababu “nilinena kwa lugha,” bali kwa sababu, “Nilikutana Naye kama Mtu!” Ndipo kamwe hutalionea Hilo haya, kuna Kitu ambacho ni kikamilifu na safi sana, na cha kweli.

¹⁵⁵ Pia kumbuka, huenda ukakutana na roho anayetenda kama Mungu. Huenda ukakutana na roho, ambaye angefanya *hili*, *lile*, ama *linginelo*; ifuate kidogo uone jinsi inavyolingana na Neno la Mungu. Unaweza kukutana na roho ambayo ingekwambia umeokoka, na kukupa hisi nzuri sana, nawe ungeweza kupaza sauti na kupiga mayowe; halafu inapofikia kwenye kulikana Neno, anawezaje Roho Mtakatifu, aliyeliandika Neno, kulikana Neno Lake Mwenyewe? Hiyo Roho haina budi kuitikia kila ahadi ya Mungu kwa “amina”! Kama sivyo, basi hujapata kukutana na Mungu, ulikutana na roho mdanganyifu. Na ulimwengu umejaa hao siku hizi!

¹⁵⁶ Lakini unapomwona Mungu akishuka na kutoa tamshi, ya kwamba atafanya jambo fulani, halafu anarudi na kufanya jambo hilo, wakati baada ya wakati baada ya wakati, basi una Roho halisi wa Mungu.

¹⁵⁷ Roho angeweza kuwa juu ya mwanadamu, Roho Mtakatifu ambaye aliandika Biblia, kisha ageuke na kukana, “Hilo si sawa, Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine”?

¹⁵⁸ Yeye alisema, “Ahadi hiyo ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali sana, na wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hilo lilikuwa ni Matendo 2:38. Roho anawezaje basi kukubali chochote tofauti na Hilo, na awe ni wa Mungu, wakati Waebrania 13:8 ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele”?

¹⁵⁹ Vipi kama mtu fulani alisema, “Loo, ninaamini Yeye alikuwa ni mwanafalsafa. Alikuwa ni mtu mzuri. Alikuwa ni nabii. Lakini kuhusu nguvu Zake. . .”

¹⁶⁰ Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi usiku na George Smith, yule mvulana anayeambatana na binti yangu, Rebekah; kijana mzuri, aliimba hapa Maskanini. Mvulana wa Kibaptisti ambaye alichukua tu. . . aliyewaambia, “Ondoeni jina langu kwenye kitu hicho! Sitaki uhusiano wowote nacho.” Na kulikuwako na msichana. . . Walikuwa na mkutano, kanisa fulani hili la Kibaptisti, juu vilimani.

¹⁶¹ Na—nao wananipinga sana, wote hao huko nje, na kuhusu kutoninii. . . Hawana neno dhidi yangu; ni dhidi ya Neno hili. Mimi, kama mwanadamu, hawawezi kusema neno dhidi yangu, sijapata kuwadhuru hata kidogo. Bali *Hilo* ndilo wanaogopa. Mnaona? Sasa tulikuwa. . .

¹⁶² Walikuwa na mkutano huu kule juu, hasa, nao walikuwa, walikuwa wawe na mmishenari atakayechukua kila usiku wa siku tatu za mwisho wa mkutano huu mkuu, huko vilimani

ambako kulikuwa si joto. Ikatokea kwamba, mmishenari huyu aliamka na akaja kwenye Marko 16, na akasema, “Kuna watu wengi siku hizi ambao hawawezi kuamini katika uponyaji wa Kiungu.” Kasema, “Nilikuwa huko India. Mimi ni Mhindi. Nami nilikuwa India wakati mtu mmoja hapa Marekani, jina lake Ndugu Branham, alipokuja.” Mchungaji akaanza kusogea. Kasema, “Mke wangu alikuwa akifa kwa kansa. Mimi nilikuwa kipofu,” ama kitu kama hicho. “Akamwombea mmoja wetu, na huyo mwingine akamwita kutoka kwenye kusanyiko, bila hata kujua lugha yetu wenyewe, kisha akanena Nguvu za Mungu.” Halafu akasema, “Tupo hapa, tumeponywa!” Vema, walijaribu kumnyamazisha. Wasingeweza kufanya hivyo. Hiyo ni, unaona, moja kwa moja katika mkutano wao wenyewe.

¹⁶³ Ndipo hata wakanyimwa chochote kile. Na baadhi ya watu hao, hata nanii wangu. . . dada wa mvulana huyu, hao wakiwa huko, hata wasingekuwa na lolote la kusema. Walitaka kujua kama hakuwa na uhusiano, kwa njia fulani wangeweza kujua.

Mmoja wa hao mama akasema, “Vema, ninaamini jambo hilo.”

¹⁶⁴ Rebekah na George wakaenda kumwona mama huyu. Naye akaenda akaleta msichana aliyekuwa na ugonjwa wa—wa. . . kitu kama kudumaa, kidogo. Kwa hiyo wakanifanya niende kule kumwona msichana huyo, hivi majuzi usiku. Ndipo nikaenda kule, maskini mama huyo alikuwa ameketi pale, ndipo nikasema, “Je! wewe ni mwaminio?”

¹⁶⁵ Akasema, “Hasha, sijui kama mimi ni mwaminio ama siye.” Vema, hakuwa amedumaa; ni pepo wa shetani tu. Hawatambui hilo. Unaona, anakupagaa, wala hujui. Anakuja, ndipo vurugu zinamshinda mtu huyo, wala hawajui.

¹⁶⁶ Wanawake wanaotembea hapa nje mtaani, wakiwa wamevaa hizi kaptura, hawatambui. Huenda wakawa, huenda wangeweza labda kuthibitisha na kuliapia, ya kwamba kamwe hawajafanya lolote ovu dhidi ya waume zao, ama kadhalika, namna hiyo. Lakini moyoni mwao, hawatambui, lakini roho wa ibilisi amewatawala. Wamepagawa naye. Kwa nini mwanamke apende kuvua nguo zake, azitoe mbele ya mwanamume? Kuna mtu mmoja tu aliyefanya hivyo, katika Biblia, nao walikuwa ni wendawazimu. Wengine hujaribu kujifunika; hawatambui. Ni janja sana, erevu sana! Inakubidi kuangalia, ujipime mwenyewe kwa Neno la Mungu, na uone mahali unaposimama.

¹⁶⁷ Msichana huyu mdogo alisema, “Loo, waliniambia ya kwamba nilibatizwa wakati nilipokuwa mdogo.” Kasema, “Sijui kama niamini upuuzi huo au la.”

Nikasema, “Hivi humwamini Yesu Kristo?”

¹⁶⁸ Basi akasema, “Vema, sijui kama ninamwamini ama la.” Akasema, “Baadhi ya huo upuuzi wa udanganyifu, siamini.”

169 Nikasema, “Vema, bila shaka, huamini upuuzi wa udanganyifu.” Nikasema, “Lakini je! unaamini ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu?”

“Loo,” kasema, “Huenda alikuwa.”

170 Nikasema, na nikasema, “Je! unaamini ni yeye yule leo, Mungu ambaye angekuokoa?”

171 Akasema, “Kuna wowote wa upuuzi huo hapo kuhusu ati kuna miujiza na upuuzi kama huo? Siamini chochote kuuhusu.”

172 Ndipo nikasema, “Ungefanyaje kama ulikuwa umeketi katika mkutano na kumwona Mungu, Roho Mtakatifu, ambaye Ndiye Mungu pekee aliyeko, akitenda kazi miongoni mwa watu; Mungu katika Ubaba, ile Nguzo ya Moto, na manabii; Mungu katika Mwanawe; kisha Mungu katika watu Wake? Ni sifa tu za Mungu, Mungu mmoja aliye mkuu ambaye anafunika Umilele.” Nikasema, “Ungeonaje kama Yeye, miongoni mwa watu Wake, aliwafanya vi—vipofu kuona, viziwi kusikia, anaangalia kwenye kusanyiko na kuwaambia watu shida zao, na kama vile alivyofanya wakati alipokuwa hapa duniani?”

Akasema, “Ninaamini ingekuwa ni uaguzi.”

173 Nikasema, “Uko katika hali mbaya zaidi kuliko nilivyodhani ulikuwa. Ingekuwa ni bora zaidi kama ungalikuwa mwendawazimu, unaona, usingewajibika.” Lakini nikasema, “Umepagawa tu na pepo mchafu.” Nikasema, “Wakati Yesu alipomwambia yule mwanamke kisimani kuhusu waume zake, wakati alipowaangalia watu na kujua mawazo yao, ungeita hayo uaguzi?” Unaona, amefungwa sana katika dhehebu, linaloitwa Lutheri, hata kitu chochote kinyume na hilo kingekuwa si cha kweli!

174 Sasa Mungu anataka mtu ambaye amefungwa katika Neno. Chochote kinyume cha hilo ni cha uongo! Yesu alisema, “Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe ni Kweli.”

175 Kulikuwako na mtu katika wakati wa kisayansi sana, jina lake Nuhu. Yeye hakulionea Neno la Mungu haya. Mungu alikutana naye, Naye akazungumza naye. Alijua ilikuwa ni Mungu. Naye akasema, “Itanyesha!” Haikuwa imenyeshwa kamwe, bali yeye aliamini itanyesha. Na imani aliyokuwa nayo, hakuona haya kuitekeleza. Ilimchukua miaka mia moja na ishirini kujenga safina, wakati ulimwengu ulikuwa unampinga. Hakulionea haya Neno la Mungu, katika siku zake. Mungu alimwoko pamoja na nyumba yake, kwa ajili ya hilo. Kulikuwa na... Jinsi lingalionekana ni jambo la kijinga kwa watu wengine; lakini, kwake, yeye alikutana na Mungu. Haidhuru huo upande mwingine ulikuwa ni wa kisayansi jinsi gani, hilo lilikuwa ni kinyume, jinsi ilivyosema, “isingewezekana, isingewezekana,” alikutana na Mungu.

¹⁷⁶ Hivyo ndivyo ilivyo wakati unapojua kwamba unazugumza na Yeye! Ungefikiri lilikuwa ni jambo la kipumbavu wakati mtu fulani... Wakati, ninajua kuna watu wachache duniani wanaoshikilia yale nisemayo kwamba ni Kweli. Kusimama hapa na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, ninaenda Arizona, huko nitakutana na Malaika saba katika kundi,” vema, kulikuwako na kundi la watu waliosimama pale kuliona likitukia. Hivi majuzi usiku, nikisema, “Los Angeles itazama baharini.” Lakini wakati umekutana na Mungu, na Mungu Ambaye hashindwi, Mungu anayefanya vile vile hasa alivyosema angefanya, daima amelifanya, wewe hulionei haya basi. Haikubidi kurudi nyuma na kuliaibikia; unaweza kuuambia ulimwengu wote. Mtu anapokutana na Mungu, anaponena Naye, na uhalisi wa Mungu unakuwa wake moyoni mwake, yeye halionei haya.

¹⁷⁷ Nuhu hakuona haya. Ilionekana ni jambo la kipumbavu kwa walimwengu wengine, bali si kwake.

¹⁷⁸ Musa, wakati alipokuwa mbele ya Farao, hakuona haya kumwambia Farao ya kwamba mambo fulani haya yangetukia, kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu. Mungu alimwambia, katika kichaka kilichowaka moto. Musa alisema, “Mi—mimi hugugumiza.” Hicho ndicho alichokuwa nacho, kigugumizi.

¹⁷⁹ Akasema, “Yule pale Aaroni anakuja. Utakuwa Mungu kwake, naye atakuwa nabii kwako. Ninajua anaweza kuongea vizuri. Lakini nitakuwa pamoja na mdomo wako. Ni nani aliyemfanya mwanadamu kuongea?” Amina. Ninapenda jambo hilo. Huyu ni Mungu. “Ni nani aliyemfanya mwanadamu kuwa kiziwi ama bubu, ama ni nani aliyemfanya mwanadamu kuongea?” Mungu amemfanya.

Akasema, “Bwana, nionyeshe utukufu Wako.”

Kasema, “Ni nini hicho mkononi mwako?”

Akasema, “Ni fimbo.”

¹⁸⁰ Kasema, “Itupe chini,” ikageuka kuwa nyoka. Kasema, “Itwae tena,” ikageuka kuwa fimbo. Amina. Yeye ni Mungu. “Weka mkono wako kifuani mwako.” Akauweka, akautoa, mweupe kwa ukoma. Kasema, “Urudishe na uutoe tena,” nao ulikuwa kama mkono huo mwingine. “Mimi ni Mungu.”

¹⁸¹ Ndipo akaenda mbele ya Farao na kusema yale Yeye alisema angesema. Akasema, “Itakuwa *hivi* na *hivi*.” Akaokota mchanga na kuutupa hewani, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, viroboto na waje juu ya nchi,” nao viroboto wakaja. Akachukua maji na kuyamwaga mtoni, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI,” na mito yote na kila kitu ikageuka kuwa damu. Akaagiza mvua ya mawe kutoka mbinguni.

¹⁸² Mwajua, katika siku za mwisho hayo mapigo yanapaswa kurudia tena. Pia kumbukeni, mzinzi, katika wakati wa Biblia, adhabu yake ilikuwa ni kifo kwa kupigwa mawe. Nalo kanisa

lisiloamini litapigwa mawe hata life, kwa mvua ya mawe, wakati mmoja ilikuwa ni njia ya Mungu ya adhabu. Yeye ataupiga mawe ulimwengu huu usioamini, kizazi hiki cha zinaa. Atakipiga mawe kutoka mbinguni, kwa mvua ya mawe ambayo kila moja lina uzito wa talanta moja, ambazo ni ratili mia moja. Kanisa la kizinzi litakufa, ulimwengu wa kizinzi utakufa chini ya adhabu ya Mungu, kwa kupigwa mawe, kama alivyofanya hapo mwanzo. Jiwekeni sawa na Mungu, enyi kanisa! Hilo ndilo linalotubidi sisi sote kufanya, kumgeukia Mungu!

¹⁸³ Yule Eliya mwenye umri wa miaka themanini, nywele za kipilipili, masharubu yenye mvi, mwenye upara, mikono iliyokonda akikaa kule nyikani, akiziangalia dhambi za watu. Mungu alisema naye asubuhi moja, kasema, “Shuka uende kule ukamwambie Ahabu ya kwamba hata umande hautashuka kutoka mbinguni mpaka utakapouagiza.”

¹⁸⁴ Ninaweza kuyaona maskini macho yake yakiangalia chini ya ndevu zake nyeupe za kipilipili, ile fimbo mkononi mwake, akishuka kwenda barabarani kama mvulana mwenye umri wa miaka kumi na sita. Akaenda moja kwa moja mbele za mfalme, na kusema, “Si hata umande utashuka kutoka mbinguni mpaka nitakapouagiza.” Hakumwonea Mungu haya wala Neno Lake; kumwambia mfalme au mtu mwingine yeyote. Hakuona haya. Haikumbidi kujificha, aseme, “Sasa Ahabu, ungekuwa ninii. . .”

¹⁸⁵ Inanikumbusha kitu kama sisi wenyewe. Ndipo nikawaambia watu, “Ninafikia mahali, ninahitaji imani zaidi.” Hiyo ndiyo sababu niko nyumbani sasa ni kupata ujazo m—mpya wa imani.

¹⁸⁶ Imefikia ambapo, inaonekana, unapowaombea watu, unaomba msamaha, “Bw. Shetani, nakusihi tafadhali uondoke na uniache ninii. . .?” Bure! Imani ina misuli, na nywele kifuani mwake. Inaponea, kila kitu kinanyamaza. Usiingie, “Bw. Ibilisi, je! utatoka?”

¹⁸⁷ “Toka hapa! Mimi ni Mwana wa Mungu, aliyeagizwa na Mungu. Achana nao!” Hiyo inamwondosha. Humwombi ibilisi msamaha, huna uhusiano wowote naye. Hulionei haya Neno la Mungu, hulionei haya agizo lako, huoni haya kwamba sisi ni nani.

¹⁸⁸ Aibu tu niliyo nayo, ni kwamba mimi ni Mbranham, huo ni uzazi wangu wa duniani. Ninaonea haya kushindwa kwangu.

¹⁸⁹ Lakini kama mtumishi Wake, sioni haya! Silionei haya Neno Lake. Kama ni madhehebu, wafalme, watawala, ama chochote kile; niko tayari tu kutoa jibu, Mungu ameagiza hilo.

¹⁹⁰ Musa alienda mbele ya Farao. Yeye hakuona aibu kumwambia ya kwamba wasingepatana na watachukua siku zake *kadhaa* huko nyikani.

Akasema, “Baadhi ya wanawake wabaki, wawachunge watoto wenu.”

¹⁹¹ Kasema, “Tutaenda sote! Hautasalia nyuma hata ukwato mmoja, tutawachukua ng’ombe wetu na kila kitu.” Hakuona haya. Kwa nini? Yeye alikuwa ameingia katika Nuru ya ukombozi.

¹⁹² Hiyo ndiyo sababu mwanamume ama mwanamke, mgonjwa ama chochote kile, akiisha kuingia katika Uwepo wa Mungu, na anajua ya kwamba Mungu amewaponya, unaingia katika Nuru ya ukombozi. Hupatani kwa jambo lolote.

¹⁹³ Ukombozi ulikuwa moyoni mwake, kwa kuwa alikuwa amekutana na Mungu ambaye alisema, “Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Yule aliyempa Ibrahimu ahadi. Na wakati, wakati wa ukombozi, wa kukombolewa, umewadia. Ninakutuma kule chini ukawatoe.” Kuna nini cha kuomba radhi, kuhusu jambo hilo?

¹⁹⁴ Farao angalimwua. Yeye alikuwa ni mwanadamu tu. Alikuwa ni mtumwa. Angeliweza kumwua. Lakini hakulionea Neno haya. Hakushuka na kupiga magoti na kumwomba Farao chochote. Alisema, “Nimekuja kuwachukua.”

Farao akasema, “Vema, huwezi kuwachukua!”

¹⁹⁵ Akasema, “Vema, basi kutakuwako na viroboto juu ya nchi, mpaka mtawapitia kwa shida.” Na hivyo ndivyo ilivyotukia.

Kasema, “Loo, Musa, waondoe!”

Kasema, “Vema. Sasa je! unatubu?”

Kasema, “Vema, mnaweza kwenda siku *kadhaa* nyikani.”

¹⁹⁶ Akasema, “Basi nzi watakuja.” Amina. Kasema, “Giza litakuja.” Kulikuwa na giza sana usingeweza kuona kutoka mahali pamoja hadi pengine.

¹⁹⁷ Na hatimaye mauti ikaja. Kutoka kwa Farao hata kwa mtumishi, ilikuwa ni mauti kwa kifungua mimba kwenye familia. Hakumwomba mtu yeyote msamaha. Yeye alikuwa ni Mwana wa Ibrahimu, aliyezaliwa katika Roho wa Mungu, akapewa agizo na Mungu, Ujumbe wa Mungu, kushuka aende huko na kuwatoa hao watu.

¹⁹⁸ Vema, hivi Mungu hawezi kuagiza kitu hicho hicho katika wakati huu, apate kumtoa Bibi-arusi kutoka kwenye kanisa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Danieli hakuwa, ama . . .

¹⁹⁹ Daudi, hakika, hakuogopa mbele ya Sauli. Wakati kila mtu alipokuwa akimwogopa Goliathi huko nje, yeye hakuogopa kumsogelea. Na akasema, “Mtumishi Wako . . .” Maskini jamaa huyu aliyeonekana kimbaombao alisema, “Mtumishi wako alikuwa akichunga kondoo za baba yake, ndipo dubu akaingia na kushika mmoja wao. Nikamfukuza mpaka huko nyikani na kumwua, kwa kombeo hili. Simba akaingia.” Loo, jamani! “Simba alikuja na kumshika mmoja wao, na akakimbia nyikani,

nami nikamwangusha kwa kombeo. Alipoamka, nikamwua.” Akasema, “Na Mungu...” Huyo mfalme aliyerudi nyuma amesimama pale, hao askari wanyonge wakidai kumtumikia Mungu wa Mbinguni, na kumwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa asimame huko nje na kuyasai majeshi ya Mungu aliye hai. Kasema, “Mtumishi wako atamwua huyo naye pia. Kwa kuwa, Mungu aliyemtia yule simba na dubu mikononi mwangu, pia atamtia huyo Mfilisti asiyetahiriwa mikononi mwangu.” Yeye hakugugumiza maneno, hakusema, “*labda* itatukia.” Alisema, “Itatukia!” Hakuona haya.

²⁰⁰ Danieli, mbele ya mfalme, hakuogopa kukaidi amri zake ya kwamba hakuna mtu atakayeomba, ila kwake tu. Akafungua dirisha na kulishusha, akaomba mara tatu kwa siku. Hakuogopa.

²⁰¹ Shadraka, Meshaki, na Abednego, hawakuogopa ile tanuru iliyowaka moto. Wakasema, “Mungu wetu anaweza kutuokoa. Mungu anaweza kutuokoa. Lakini kama hatuokoi, hatutaisujudu sanamu yako.” Hawakulionea haya. La, bwana. La, bwana. Hakika hawakulionea haya, kwa sababu walijua.

²⁰² Samsoni hakuona haya mbele ya Wafilisti. Wakati elfu moja walipomkimbilia, aliokota taya la nyumbu. Na hizo chepeo, zilikuwa na unene wa kama inchi moja na nusu, za shaba. Aliwaua elfu moja kwalo, na angali alikuwa na taya hilo mkononi mwake. Hakutahayari. Alitwaa tu kilichokuwa mikononi mwake, akaenda kufanya kazi nacho. Alijua ya kwamba Roho wa Mungu alikuwa juu yake. Alijua alizaliwa Mnazarayo. Alijua ya kwamba hakuna kitu kingalimsumbua. Yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Mradi tu alikuwa katika mapenzi ya Mungu, hakuna kitu kingeliweza kusimama mbele zake, haidhuru ni wafalme wangapi ama Wafilisti, ama wowote wale walioinuka. Kweli.

²⁰³ Yohana hakulionea haya Neno la Mungu lililomjia nyikani, na kumwambia aende akabatize kwa maji. Hakuona haya kusema, “Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu,” kwa kuwa Roho wa Mungu alikuwa juu yake. Hakuona haya mbele ya makuhani.

²⁰⁴ Hakulionea haya Neno la Mungu wakati alipoenda kwa Herode. Mke wa Filipo alikuwa akiishi na Herode. Akaenda moja kwa moja mbele za mfalme huyo! Mzee huyu mwenye nywele za sufu kutoka kule nyikani, alitoka huko, bila elimu au chochote kile, na akaenda moja kwa moja mbele ya Herode, na kusema, “Si halali kwako kumchukua!” Hakulionea haya Neno la Mungu. Hakika. Kweli kabisa yeye hakulionea aibu.

Stefano, hakulionea haya Neno la Mungu.

²⁰⁵ Kwanza, wapentekoste kule juu kwenye ile Siku ya Pentekoste, walipokusanyika kwenye chumba cha juu, Roho

Mtakatifu alishuka juu yao, kwa ahadi ya Mungu. Luka 24:49 ilisema:

... tazama nawaletae juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni. . . mjini Yerusalemu, hata mvikwe uwezo utokao juu.

²⁰⁶ Na ahadi ile ile ambayo Neno la Mungu liliwaahidi, “Tazama, nawaletae juu yenu ahadi ya Baba Yangu, lakini kaeni humo; msipate theolojia tena wala elimu zaidi, na kadhalika, ngojeni hata mvikwe Nguvu.” Na wakati Nguvu hizo kutoka Mbinguni zilipokuja, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, hawakuionea haya Injili.

²⁰⁷ Petro alisimama, akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu. Enyi wanaume, kwa mikono ya watu wabaya, mmemsulibisha Mfalme wa Amani, ambaye Mungu amemfufua kutoka katika wafu. Nasi ni shahidi. Kwa maana hili ndilo Yoeli alisema lingetukia katika siku za mwisho, ‘Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.’” Hakuionea haya Injili.

²⁰⁸ Maskini Stefano, kama nilivyomtaja dakika chache zilizopita, wakati alipopitia pale kama ki—ki—kimbunga. Yeye hakuwa mhubiri. Alikuwa ni shemasi tu, bali alishuhudia kila mahali juu ya ufufuo. Alikuwa amekutana na Mungu. Na ni kama tu. . .

²⁰⁹ Ati ujaribu kumzuia? Vema, ilikuwa ni kama kujaribu kuizima nyu—nyumba, nyumba inayoteketea, kuuzima moto wake, kwenye siku yenye upepo, kukiwa kukavu. Mbona, kila wakati upepo ulipovuma, uliwasha tu moto mwingine.

²¹⁰ Walimkokota mbele ya Baraza la Wazee. Mnaweza kutambua kwamba hiyo ni nini? Hilo ni kama Baraza la Ekumenia. Dini zote zinaelekea, zinaingia chini ya Baraza la Ekumenia. Wote wakielekea kule chini ya Baraza la Wazee. Mafarisayo, Masadukayo, Maherodia, wowote wale, iliwabidi waingie kwenye baraza hilo. Nao wakamchukua kwa nguvu, sio tu shirika moja, bali baraza kuu lilimchukua kwa nguvu. “Tutamtisha mpaka ajute.”

²¹¹ Alipoenda kule, asubuhi hiyo, Biblia ilisema uso wake ulionekana kama wa Malaika. Akasema, “Wanaume na ndugu zangu, hebu niseme nanyi. Baba zetu walikaa Mesopotamia kabla hawajakuja Harani,” kadhalika. Angeendelea na kutoa Maandiko. Ndipo alipomaliza, Roho alishuka juu yake, akasema, “Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa mioyo wala maskio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu, kama baba zenu walivyofanya, nanyi vivyo hivyo.” Yeye hakuionea haya Injili, hakulionea haya Neno. Hakutahayari mbele ya Baraza lolote la Wazee. La.

²¹² Paulo alisema mbele ya Agripa. Akiwa Myahudi, aliyefunzwa chini ya Gamalieli, alikuwa ni mashuhuri sana. Lakini siku moja, akienda zake Dameski, alikuja Uweponi,

akakutana na Mungu. Malaika alishuka kutoka Mbinguni, katika umbo la Nguzo ya Moto, Nuru iliyomwangusha sakafuni. Akasimama, na kusema, “U Nani Wewe, Bwana?”

Naye akasema, “Mimi ni Yesu.”

²¹³ Akasimama mbele ya Agripa, akarudia hadithi hiyo tena. Akasema, “Siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa maana ni nguvu za Mungu kwa wokovu, kwa kila aaminiye.” Hakika.

²¹⁴ Sasa, enyi marafiki, tumeshuka tukaja na mtu, kote katika wakati, lakini tumepitiliza muda.

²¹⁵ Lakini hebu niseme jambo hili. Mtu ambaye wakati mmoja amekutana na Mungu, ambaye ni Neno, nalo Neno limefanywa dhahiri na kudhihirishwa kwake, hakuna aibu kuhusu jambo hilo. Hutahayarishwi. Hainitahayarishi mimi kusema ninaamini kila Neno la Mungu. Hainitahayarishi wakati Bwana ananiambia niseme lolote, wewe nenda uliseme na kulifanya; hainitahayarishi mimi kusema ya kwamba nimejazwa na Roho Mtakatifu; hainitahayarishi kusema ya kwamba nimenena kwa lugha zingine; hainitahayarishi kusema ya kwamba Bwana wetu amenionyesha maono; hainitahayarishi kusema ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

²¹⁶ “Mnapoletwa mbele ya watawala na wafalme, kwa ajili ya Jina Langu, msifikiri-fikiri yale mtakayosema, kwa maana mtapewa kwenye saa hiyo. Si ninyi msemao, bali ni Baba Yangu aishiye ndani yenu. Lakini kila atakayenionea Mimi haya na Neno Langu, katika kizazi hiki, huyo nitamwonea haya mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Mungu na atusaidie tusione haya, bali atusaidie kuwa ushuhuda ulio hai.

²¹⁷ Kila mtu katika Agano la Kale, wakati hao manabii walipokuja, wao walifanyika—walifanyika Neno lililo hai. Walikuwa ni Neno. Yesu alisema waliitwa miungu, nao walikuwa hivyo, kwa sababu Neno la Mungu liliwajia. Wanasema, “Ni BWANA ASEMA HIVI.”

²¹⁸ Na mwanafunzi yeyote wa Kristo ambaye amekutana Naye katika ukombozi, na wokovu umeingia moyoni mwake, yeye ni mrithi wa Mungu. Nasi tunapaswa kuishi maisha ya namna gani, na tunapaswa kuenenda jinsi gani, na tunapaswa kuzungumza namna gani, kama Mungu anajiwakilisha kupitia miili yetu inayopatikana na mauti? Ni nani angeweza kuona haya kwa ajili ya jambo hilo?

²¹⁹ Kama nikifikia mahali ambapo nilikuwa kwenye kikosi cha polisi hapa Jeffersonville, nishuke mtaani, kwa mamlaka yote, nisingeonea aibu mji huu. Ningekuwa sehemu ya mji huu. Ningekuwa polisi, sehemu ya mji, kuweka utaratibu na mwenendo. Kama mtu akiipita taa nyekundu, nisingeona haya kumwambia ametenda kosa, nimpe ilani. Hiyo ni kazi yangu, maana ni—ninalipwa na mji. Ninaishi kwa mji. Nina mamlaka kutoka kwa mji. Haidhuru kama alikuwa amelewa, ama shida

yake ilikuwa ni nini, wataniunga mkono. Ninasimama kwenye wajibu wangu, maana mimi ni polisi na ama . . . Nimechaguliwa, ama kuwekwa hapa na kupewa mamlaka kufanya jambo hili. Unapaswa kuchukua sheria na haki, na kadhalika, na kuona kwamba imetekelezwa vizuri.

²²⁰ Basi, kama mimi ni Mkristo na nimejazwa na Roho Mtakatifu, nikiuvaa ushuhuda wa kufufuka kwa Yesu Kristo, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, usimwache shetani yeyote ajaribu kukusukuma huku na huko, aseme, “Usifanye *hili* na usifanye *lile*.” Unalifanya. Mungu amekupa ninii . . .

²²¹ Mnaona, hatuna nguvu. Huyu polisi hana nguvu za kusimamisha hata gari moja. Ni kuhusu . . . wakati mwingine ni magari ya nguvu farasi mia tatu ama mia nne, angefanya nini juu ya jambo hilo? Bali ana mamlaka.

²²² Na hivyo ndivyo ilivyo Kanisa. Tuna mamlaka, kwa ufufuo wa Yesu Kristo na Neno Lake lililoahidiwa, haleluya, “Mambo niyafanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya; na mengi kuliko haya mtayafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba.”

²²³ Msimwonee haya katika kizazi hiki; chenye dhambi, kilicho na fadhaa, kizazi cha mwisho kitakachopata kuwa duniani, hiki chenye dhambi, cha uzinzi, na kilichojaa vidonda vitokavyo usaha. Yote, kila kitu ambacho kimekuwa ni cha heshima kimekuwa ni cha aibu. Siasa za kitaifa, uchafu! Mataifa yamesambaratika.

²²⁴ Huko mbali sana katika misitu ya Afrika, kwenye safari za kuwinda, iliwabidi kuchukua redio za masafa marefu wapate kumsikia Elvis Presley, Pat Boone, na hao jamaa wenye hiyo roki na twisti. Nao wenyeji, wakijaribu kuwaangalia wanavyotenda, wakivitikisa vichwa vyao na kufanya hivyo, wenyeji walisimama na kuwaangalia. Lakini, unaona, hao si Wamarekani kama vile Pat Boone, na Elvis Presley, na Ricky Nelson, na hao jamaa walivyo. Hao si Mayuda wa aina hiyo, bali wao ni . . . Mnaona, ni pepo. Na pepo huyo hayuko tu Marekani, ameenea kote ulimwenguni, apate kuwaleta kwenye vile vita vya Harmagedoni. Wanafanya jinsi hiyo, kama wao ni ninii . . . Taifa lolote wanalotoka, Afrika, India, popote pale, ushenzi huo na upuuzi umeenea kote duniani, kwa kuanzishwa tu na mtu mmoja.

²²⁵ Vivyo hivyo na Injili na Nguvu za Mwenyezi Mungu, zimeenea kote ulimwenguni! Na wakati wa kutengana unatukia sasa, wakati Mungu anamwita Bibi-arusi, naye shetani analiita kanisa. Jalia niwe sehemu ya huyo Bibi-arusi.

Na tuombe.

²²⁶ Mungu mpenzi, tunaona maandiko ya mkono ukutani, Bwana. Tuko katika wakati wa mwisho. Tunajua ya kwamba kuna mambo makuu yako mbele, bali hata hivyo mahali fulani, mahali fulani kutoka kwenye machafuko haya hapa nje, kungali

kuna watu waaminifu waliokusudiwa Uzima. Linge kuwa ni jambo lisiloweze kana kwa mtu mmoja ama wawili; bali, Mungu, sisi sote pamoja, jalia tuisambaze kwenye kila pembe tuwezayo, habari njema ya kwamba Yesu yuaja, na, unaona, tusambaze Mkate kidogo twendapo, Neno dogo. Popote walipo Tai, wataki fuata Chakula hicho. Kama kimekuja kwa kanda, ama kama kimekuja kwa neno ama ushuhuda, Tai wataki fuata mpaka kwenye makao Yake makuu. Kwa kuwa imeandikwa, “Ulipo Mzoga, hapo Tai watakusanyika.” Mpenzi Yesu, tunajua ya kwamba Wewe Ndiwe huo Mzoga tunaoula. Wewe ni Neno, nalo Neno lilifanyika mwili likakaa kwetu. Tunaomba, Mungu, ya kwamba tunapolisambaza Neno, ya kwamba Tai wa Kweli watalipata.

²²⁷ Jalia tusione haya tunaposimama mbele ya watu; waovu, wasiojali, wa kidini, chochote kile. Kama vile Paulo alivyomwambia Timotheo:

...Na tuwe tayari, wakati ufao na wakati usiofao; karipia, kemea na...kwa uvumilivu wote na mafundisho.

Kwa sababu utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajiipatia pamoja waalimu makundi makundi; kwa kuwa wana masikio ya utafiti;

Nao watageuzwa...wasisikie yaliyo kweli,... watazigeukia hadithi za uongo.

²²⁸ Mungu, tunaishi kwenye siku hiyo. Umenijalia kuishi muda mrefu vya kutosha kuona jambo hilo likitukia. Kwa kuwa, hilo liko papa hapa kwenye jiwe la pembeni la maskani hii leo hii, ya miaka thelathini na mitatu iliyopita.

²²⁹ Mungu, mbariki kila mmoja hapa ndani. Kama kukiwako na mmoja hapa, Bwana, ambaye hayuko tayari kukutana na Wewe, kwamba hawawezi kamwe kukubaliana na Neno Lako, nao hawajakutana na Wewe uso kwa uso na kujua ya kwamba Wewe hutokani na namna fulani ya tendo la—la—la kuwaziwa tu, kama vile ungeliwazia kanuni ya imani ama chochote kile, bali wamekutana na Mungu aliye hai; na kama hawajafanya jambo hili, Bwana, jalia walifanye sasa hivi.

²³⁰ Mimi—mimi ninaamini Wewe uko—Wewe uko karibu sana kwenye saa hii. Sijui hao ni akina nani. Hata sijui kama kuna yeyote hapa, bali ninajisikia tu kuongozwa kukuomba Wewe. Si kwamba watu wanisikie, kwa kuwa huo ungekuwa ni unafiki. Mungu na anizuie. Sitaki kuwa mnafiki. Lakini ninaomba jambo hilo kwa uaminifu moyoni mwangu, Bwana.

²³¹ Yeyote yule mwanamume au mwanamke ambaye unasema naye asubuhi ya leo, jalia kwa unyenyekevu wasione haya, bali huko chini kabisa ndani ya moyo wao wakupokee Wewe sasa, wakija jioni ya leo na kubatizwa katika Jina

la Yesu Kristo, wakilifuata kila Neno, kila Neno; kama wamebatizwa vinginevyo, ama kunyunyiziwa, kumwagiliwa. Kumbuka (tunakumbuka, Bwana) ya kwamba Wewe ulisema, “Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Kitabu hiki, aongeze neno moja Kwake, ataondolewa sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Ingawa anajaribu, anakuja, anaweka jina lake kwenye kitabu, ha—haitafaa kitu. Jalia tuwe waaminifu na wanyenyekevu.

²³² Sasa wako mikononi Mwako, Bwana. Fanya nao upendavyo, kwa kuwa ni Wako. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

²³³ Sasa wakati tumeinamisha vichwa vyetu, ninawatakeni mwazie kwa dhati sana sasa. Naomba radhi, kwanza, kwa kuchelewa kama dakika kumi na tano. Sasa tunataka kuvumisha. Na wewe wazia tu moyoni mwako sasa, “Je! kweli mimi nimekutana na Mungu?” Sasa hebu wazia tu jambo hilo kwa uaminifu sasa. Maana, haitakuwa ni mara nyingi labda mpaka . . . Huenda ikawa ndio wakati wa mwisho sasa, ambapo tutakutana kabla ya Kuja Kwake. Kumekaribia, enyi marafiki. Kila Andiko, inaonekana, karibu limetimizwa tu. Na huenda ikawa, kwako wewe ama kwangu mimi, huenda hii ikawa ndiyo nafasi yetu ya mwisho. Huenda tukaondoka kabla ya usiku.

Nitaambatana Naye, Naye njiani kote.

Ninaweza kumsikia, “Je! unanionea haya
Mimi na Neno Langu?”

Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu . . .

²³⁴ Sasa hebu wazia tu umelala kwenye kitanda chako cha mauti sasa. “Naweza kumsikia . . .” Huenda wakati huo ikawa umechelewa sana, bali sasa hivi hujachelewa.

“Uchukue msalaba wako, na,” huenda
ikakubidi kujitolea sasa, “unifuata.”

Sasa, katika moyo wako, jibu hili:

Nitaambatana Naye shambani,
Nitaambatana Naye shambani,
Nitaambatana Naye shambani,
Nitaambatana Naye kote . . .

²³⁵ Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu na tuinue tu mikono yetu na kusema:

Nitaambatana Naye hukumuni,

Sasa, hiyo ndiyo inayoendelea sasa hivi, Yeye anatuhukumu.

Nitaambatana . . .

Bwana, je! Unaniona na hatia? Basi, nisamehe.

. . . hukumuni,

Unaniona vipi asubuhi ya leo, Bwana?

...pamoja Naye hukumu-...

Nichunguze, Bwana, uone kama kuna kitu chochote kichafu ndani yangu.

...pamoja Naye, pamoja Naye njiani kote.

²³⁶ Baba, tunakushukuru asubuhi ya leo kwa ajili ya mikono hii yote. Sikuona mtu mmoja ila wale walioinua mikono yao juu. Ninakushukuru, Bwana. Na—naamini hata Wewe hukuona, Bwana. Hakuna mmoja ambaye hakuinua mikono yao juu, wako tayari kupitia hukumuni. Tuhukumu, Bwana. Na kukiweko na jambo lolote baya ndani yetu, tusamehe hilo, Baba. Tupe rehema Yako, kwa kuwa hatutaki kukutana na hukumu Yako isipokuwapo rehema. Kwa hiyo, rehema ipo sasa, kwa hiyo tunaomba, Mungu, ya kwamba utatuhukumu na kutusamehe dhambi zetu, kulingana na Neno Lako na ahadi Yako. Na jalia tukuishie siku zote za maisha yetu, bila ya kuionea haya Injili.

²³⁷ Sasa, Baba, kama ni mapenzi Yako, tunaanza Jumapili tatu mfululizo sasa, za mikutano. Iandae mioyo yetu kwa ajili yake, Bwana. Niandae, Ee Mungu. Mimi ndiye ninayesimama nikiwa ninakuhitaji kwa kina sana. Ninaomba ya kwamba utaniongoza na kunielekeza katika mambo ambayo ningepaswa kuyafanya na kuyasema, katika siku hizi zijazo.

²³⁸ Mwongoze na kumwelekeza Ndugu yetu wa thamani Neville, yule mtumishi Wako shujaa, Bwana; na pia Ndugu Mann, na mashemasi wa kanisa, na wadhamini, na kila mtu anayekusanyika hapa.

²³⁹ Tuandae, Bwana, kusudi tuweze, kwa njii—njia halisi ya Ukristo, kukuletea wenye dhambi, na kuwaleta wafuasi wa kanisa kufikia kumjua Mungu tunayemjua, ambaye tumekutana Naye kibinafsi, jalia Yeye awe ni Mungu wao, pia. Sasa, Baba, hili hatuwezi kufanya, hatuwezi kuwatuma mle. Lakini Wewe, Roho Mtakatifu, tenda kazi miongoni mwa watu, wafuasi wa makanisa.

²⁴⁰ Na kama tukio dogo nililokuwa nalo pamoja na Wewe hivi majuzi asubuhi, “Nenda ukamtafutie Mwanangu Bibi-arusi. Mchukue kutoka miongoni mwa watu, miongoni mwa makanisa. Mtoe huyo Bibi-arusi.” Nijalie, katika maombi sasa, Bwana. Mtume huyo Rebeka; mimi nitajaribu kuwa Elieza. Nisaidie kuwa mtumishi mwaminifu. Na jalia Mungu wa Mbinguni amtume Malaika Wake mbele zangu, mbele zetu, ili kwamba tutavikusanya vitu hivyo pamoja na kumchagua Bibi-arusi ambaye Yeye amemchagua. Tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

²⁴¹ Sasa, ninasikitika nimewachelewesha kidogo. Zimepita dakika ishirini na tano. Ningepaswa kuwa nimeondoka humu, dakika ishirini na tano zilizopita. Lakini, sasa, mnaupenda wimbo huo wa kale, “Peleka Jina la Yesu”? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Huo si ni mzuri? Nimeuimba huo sasa kwa

miaka thelathini na mitatu, kama wimbo wa kufumukana. Ubatizo wa maji, “Ninasimama kwenye kingo zenye tufani za Yordani.” Nami ninafikiri huu ni mzuri sana, “Lipeleke tu kokote uendako!”

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini . . . (Sasa peana mikono na mtu fulani
karibu nawe.)
Jina la thamani, Jina la thamani, Loo ni tamu
jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;

²⁴² Sasa kumbukeni ibada ya usiku wa leo, saa moja na nusu, saa moja na nusu usiku wa leo. Sasa hebu tuimbe aya hii moja, unaona.

Peleka Jina la Yesu
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Majaribu yanapokuzunguka . . . (Unafanya
nini basi?)
Litaje tu Jina hilo katika maombi.
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;

²⁴³ Kuna yeyote aliyekuja kubatizwa baada ya ibada hii? Kama wapo, inueni mikono yenu. Kuna mtu wa kubatizwa? Wawili, vema, watakaobatizwa mara baada ya ibada hii. Kama wengine wenu, yeyote wenu anayetaka kubatizwa, tutakuwa na ibada ya ubatizo katika kila moja ya ibada hizi. Jambo pekee likupasalo kufanya ni kuomba. Tuko tayari kukubatiza. Hiyo ni kazi yetu, kukubatiza katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Ni kazi yetu kufanya hilo. Nasi tutafurahia kufanya hivyo, wakati wowote. Ninyi ambao mtabatizwa, nendeni tu vyumbani, mara baada ya ibada, nasi tutaendelea moja kwa moja na ubatizo wa maji. Mtu yeyote anayetaka kuwafuata, utakuwa na hakika ya kwamba tupo hapa . . . kama umetubu dhambi yako nawe umemkubali Yesu kama Mwokozi wako.

²⁴⁴ Umekuwa Mkristo kwa miaka mingi, wala hujaona Nuru, nayo Nuru ya ukombozi imekuja sasa. Mwanamke, Bibi-arusi ambaye hana budi kulichukua lile Jina! Yesu alisema, “Nilikuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea. Lakini atatokea mtu atakayekuja katika jina lake mwenyewe, nanyi mtampokea,” hilo ni dhehebu lako.

²⁴⁵ Mwana yeyote huja katika Jina la baba yake. Nimekuja katika jina la baba yangu. Ninyi watu mmekuja katika jina la baba yenu.

²⁴⁶ Basi Jina Lake lilikuwa ni lipi, Jina la Baba ni lipi? Yesu! Yeye, “nilikuja katika Jina la Baba Yangu, hamkunipokea.” Sasa Bibi-Arusi Wake atakuwa na Jina Lake, bila shaka.

²⁴⁷ Nilimchukua mwanamke, jina lake Broy, naye akawa Branham.

²⁴⁸ Yeye anakuja kumchukua Bibi-arusi, kuwa na hakika na ukumbuke jambo hilo unapokuja kwenye kidimbwi.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

²⁴⁹ Naye Ndugu Vayle hapa si mgeni kwetu. Yeye ni ndugu wa thamani sana, amekuwa pamoja nami katika mikutano mingi, yeye na mke wake. Naye pia sasa ndiye mwandishi wa mahubiri na kadhalika yanayoingizwa kwenye kitabu. Ndugu Vayle, naomba uturuhusu tufumukane kwa maombi, tunapoviinamisha vichwa vyetu. [Ndugu Vayle anaomba—Mh.]



KUONEA HAYA SWA65-0711
(Ashamed)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 11 Julai, 1965, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org